

KUIFANYA BIBLIA KUWA YAKO

KUIFANYA BIBLIA IWE YAKO	7
UTANGULIZI	7
KUANZA.....	9
SOMO LA KWANZA —SEHEMU 1.....	13
MAZOEZI:	13
FUNDISHO:.....	13
➤ MAFAFANUZO:.....	13
MAZOEZI:	14
ORODHA YA VITABU VYA AGANO LA KALE NA VIFUPI VYAKE (39) (Agalia ukurasa 3).....	15
Somo 1 – Sehemu 1	15
VITABU VYA AGANO JIPYA NA VIFUPI VYAKE (27).....	15
SOMO LA KWANZA — SEHEMU 2.....	15
MAFUNDISHO:	16
MAZOEZI:	17
SOMO LA KWANZA —SEHEMU 3.....	18
MAZOEZI:	18
MAZOEZI:	19
MATUMIZI:.....	20
MAOMBI:	20
SOMO LA KWANZA —EHEMU 4.....	20
MAZOEZI:	21
MAOMBI:	21
MAZOEZI:	22
MATUMIZI:.....	23
MATUMIZI:.....	24
SALA:	24
SOMO LA KWANZA —EHEMU 5.....	24
MAZOEZI:	24
MASWALI:	24
MATUMIZI:.....	25
SALA:	25

KUIFANYA BIBLIA KUWA YAKO

SOMO LA PILI — EHEMU 1.....	25
UTANGULIZI:	25
FUNDISHO:	26
➤ MAFAFANUZI:	26
MAZOEZI:	27
MAZOEZI:	27
SOMO LA PILI — SEHEMU 2.....	28
FUNDISHO:	28
MAZOEZI:	28
MATUMIZI:	29
SALA:	29
SOMO LA 2 SEHEMU YA 2.....	29
MAZOEZI:	30
SOMO LA PILI — SEHEMU 3.....	31
FUNDISHO:	31
MAZOEZI:	31
➤ MAFAFANUZI:	32
SOMO LA PILI — SEHEMU 4.....	33
MAFUNDISHO:	33
MAZOEZI:	35
MATUMIZI:	35
SALA:	37
SOMO LA PILI — SEHEMU YA 5.....	37
MAFUNDISHO:	37
SOMO LA TATU — SEHEMU 1.....	39
ZANA #3:	39
MAZOEZI:	39
SOMO LA TATU — SEHEMU 2.....	40
MAFUNDISHO:	40
MAZOEZI:	41
SOMO LA TATU — SEHEMU YA 3.....	41

KUIFANYA BIBLIA KUWA YAKO

ZANA #4:	41
MAFUNDISHO – (matumizi ya itifaki ya Biblia):	42
MAZOEZI:	42
MAZOEZI:	42
SOMO LA TATU — SEHEMU YA 4.....	43
MAFUNDISHO (Matumizi ya Itifaki ya Biblia):.....	43
MAZOEZI:	43
MATUMIZI:.....	44
SALA:	44
SOMO LA TATU — SEHEMU 5.....	45
MAFUNDISHO - (Nyongeza katika matumizi ya itifaki):.....	45
ZOEZI:	45
MARUDIO:.....	45
SOMO LA NNE — SEHEMU YA 1	47
UTANGULIZI:	47
FUNDISHO:	47
ZANA #5:	48
ZOEZI:	48
SALA:	49
SOMO LA NNE — SEHEMU 2.....	49
FUNDISHO:	49
ZOEZI:	50
MATUMIZI:.....	50
SALA:	51
SOMO LA NNE — SEHEMU YA 3	51
MAZOEZI:	51
ZANA #7:	52
ZOEZI:	52
SALA:	53
SOMO LA NNE — SEHEMU 4.....	53
MARUDIO:.....	53

KUIFANYA BIBLIA KUWA YAKO

ZOEZI:	53
FUNDISHO:	54
ZOEZI:	55
FUNDISHO:	56
➤ MAANA:	58
SALA:	59
SOMO LA TANO—SEHEMU YA 1	60
FUNDISHO: –	60
1.Maombezi.	61
2. Kukiri	61
3. Shukrani	61
4. Maombezi	62
SOMO LA TANO — SEHEMU YA 2	62
FUNDISHO:	62
ZOEZI:	62
SOMO LA TANO — SEHEMU YA 3	63
FUNDISHO: Maombi.....	63
2.UKIRI:.....	63
SOMO LA TANO — SEHEMU YA 4	64
FUNDISHO: Maombi.....	64
SHUKRANI:	64
ZOEZI:	65
SOMO LA TANO — SEHEMU 5	65
FUNDISHO:Maombi	65
5 ZOEZI:	66
SOMO LA SITA — SEHEMU YA 1	66
FUNDISHO:	66
ZOEZI:	67
SOMO LA SITA— SEHEMU YA 2	68
FUNDISHO: Maombi.....	68
ZOEZI:	69

KUIFANYA BIBLIA KUWA YAKO

SOMO LA SITA — SEHEMU 3.....	69
FUNDISHO:	69
ZOEZI:	69
SOMO LA SITA — SEHEMU YA 4	70
ZOEZI:	70
SOMO LA SITA ~ SEHEMU YA 5	71
ZOEZI:	71
ZOEZI:	71
MARUDIO	72

KUIFANYA BIBLIA KUWA YAKO

***Safari katika moyo wa mungu* IMEANDIKWA NA JACKIE
“MOYONI MWANGU NIMELIWEKA NENO LAKO NISIJE
NIKAKUTENDA DHAMBI...”
ZABURI 119:11**

ii

© 2007 FullValue Ministries

Isipokuwa ilezwe viginevyo, Nukuu zote za Biblia zimechukuliwa toka
BIBLIA TAKATIFU, NEW
INTERNATIONAL VERSION ®. Copyright © 1973, 1978, 1984 by
International Bible
Society. Imetumika kwa ruhusa ya Zondervan. Haki zote zimehifadhiwa
Kimechapwa Jamuuri ya Muungano ya Marekani ISBN.

Haki zote zimehifadhiwa na waariri. Muariri amehakikisha kuwa yote
yaliyo ndani ya kitabu hiki ni ni ya asili. Usichakachue haki na kazi
halali ya mtu mwingine. Hakuna sehemu ya kitabu hiki inayoruhusiwa
kutolewa kwa njia nyingineyo pasipo kibali cha waariri.

www.xulonpress.com

UTANGULIZI

Siku moja mtu mmoja alinunua gari mpya. Muuzaji wa gari hilo alitumia mda mrefu sana akielezea vyombo vingi visivyo hesabika vilivyotengeneza gari hili la kisasa. Gari hili lilikuwa na kengere na firimbi za wakati uliopo. Kulikuwa na uwezekano kuwa utalam uliotumka kutengeneza gari hilo ulikuwa wa kudumu kwa mda mrefu. Baada ya kufunga mkataba, mmiliki mpya alichukua gari lake akaliegsha nje ya nyumba yake. Familia yake ilitamani sana waingie kwenye gari hilo na kuliendesha kwa mara ya kwanza. Hata majirani zake walikuja walitamani kusafiri kwenye gari hilo. Mwenye gari alikuwa haongei kitu huku akishangaa na kufurahia uzuri wa gari lake.

Alikuwa na akitafakari jinsi atakavyo tembelea maeneo mbalimbali akionyesha kuwa sasa ana gari. Alijione kuwa yuko juu ya ulimwengu wote, na hakuna jambo linge mzuia kuendesha gari lake. Pamoja na ndoto zake hizo siku baada ya siku, gari liliendelea kuegeshwa hapo mahali ambapo hapakuwa na usalama wa kutosha kutokana na hali ya hewa ya hapo kuwa mbaya. Mvua na barafu viliendelea kunyeshea gari hilo masika; na jua kali wakati wa kiangazi viliendelea kupiga juu ya bodi ya gari hilo. Pasipokujali hayo yote, mwenye gari aliendelea kulionsha na kulipaka rangi. Familia yake na majirani waendelea kushangaa kwanini hakuingiza gari kwenye nyumba ya magari au mahali penye paa. Walianza kukata tamaa na ndoto zao za kusafiri mbali wakitumia gari lao hilo.

Siku moja majirani zake walimjia wakati akisang'arisha aking'arisha gari hilo, wakamuuliza kuhusu gari lake. Mmoja wao akamuuliza sababu ya kutotunza gari lake kwenye jengo na kwanini hajawi kuitumia. Mmiliki wa gari mwenye majidai alisita kujibu; lakini kwa uso wa aibu alikubali na kusema kuwa hakujua kuendesha gari. Hakuna aliyekuwa amemwelekeza jinsi gari linavyofanya kazi. Hakuwa na ufahamu wowote jinsi ya kutumia vifaa vizuri vya gari yake. Alichofahamu ni kuwa vilikuwa vimeunganishwa kwenye vitu alivyonunua pamoja na gari. Hakuna aliwai kumfundisha kuhusu kitabu cha matumizi na wala alikuwa hajaisoma. Alitaka kufurahia kuendesha gari lakini hakujua hata mahali pakingiza ufunguo, wala jinsi ya kuwasha gari. Hakujua hata mambo ya msingi juu ya kuendesha gari, jambo lililo mfanya ajione mjinga kwa kwa kununua gari hilo. Asingeweza kulirudisha. Angelitunza lakini bahati mbaya hakujua jinsi ya kuitumia. Jambo lililo kuwa njozi njema, sasa analichukia na kujaribu kulihepuka. Baada ya kushirikisha jirani yake juu ya tatizo lake hilo, alimuuliza kama angemuonyesha baadhi ya mambo muhimu ambayoyangemwezesha kufurahia gari lake. Baada ya hapo walifungua, wakasoma kitabu cha maelekezo. Wakaingiza ufunguo wakawasha gari. Jirani yake akamfundisha mambo muhimu kwenye gari lake, akajidunza jinsi ya kutumia vifaa hivyo, na kumudu usukani wakati akiendesha gari,

akajifunza jinsi ya kukwepa magari mengine. Baada ya mda mfupi akaanza kuendesha gari mwenyewe na hatimaye kutimiza ndoto yake na ya familia yake. Familia yake ilianza kupanga safari za kuvinjari nchi. Baadae alijiunga kwenye kikundi cha wamiliki wa magari ili kupata ushauri kuhusu usalama katika safari za mbali. Alianza kuwa mtu aliye huru, hakushitakiwa tena na dhamira yake, badala yake alianza kuishi kwa mipango na matumaini ya wapi gari lake linge mpeleka siku siku na wakati wowote! Je, Uliishajisikia kwa jinsi hiyo? Uliishanunua kitu lakini hukufaidi kitu hicho kwasababu ilikuwa vigumu kutambua kitabu cha maelezo? Masomo haya *Kufanya Biblia iwe yako*, yameandaliwa yakikuwaza wewe.

Labda bado hujamiliki Biblia na hii ni mara yako ya kwanza kuwa na ufahamu juu yake. Au una Biblia lakini hujafundishwa jinsi ya kuisoma. Matokeo yake umekaa nayo bila kuisoma ukiwa imengia ndani ya shelfu ya vitabu. Ulijua kuwa huko huko, na labda umekuwa ukiipangusa vumbi baada ya mda Fulani au kuihamisha toka mahali kwenda mahali. Umekuwa ukijisikia deni kwa kutoisoma lakini umekuwa ukishindwa wapi uanzie kwa namna gani hatimaye ukaamu kuachana nayo. Unaalikwa kushiriki. Unachotakiwa kuja nacho ni moyo wako uliowazi na wenye shauku ya kutembea kwenye Moyo wa Mungu ulio wazi. Wakati ukiendelea kusoma, Mpe nafasi ya kuingia kujenga uhusiano na wewe. Furahia safari. Kuna mengi ya kujifunza ukiwa njiani. Changamkia na kufurahia jambo hilo. Sasa hebu tuwashe gari!

KUANZA

Unaanza safari mpya ambayo itabadilisha maisha yako. Masomo haya ya kujifunza Biblia yameandaliwa yakiwa na wewe katika mawazo yake. Safari yako itakuwa ya pekee kwako pia kwa sehemu itategemea utayari wako na upendo wako wa kutaka kukua katika kufahamu Kitabu hiki Biblia. Kujituma kwako katika masomo haya yatakuhakikishia kukua kwako kama Mungu asemavyo na wewe kupitia Neno lake. Unahimizwa kuwa na vitu vitano sawa na ilivyoshauriwa, hivi vitakuwa

rejea zako kadiri unavoendelea na masomo, na utavitumia kila siku ya kujifunza Biblia ili kukuza ufahamu wako kimasomo na uzoefu.

1. Kusoma Biblia: *Kufanya Biblia kuwa yako*

2. Kama unataka kununua Biblia mpya. Angalia Biblia yenye yafuatayo:

- a. yenye yaliyomo yenye orodha ya vitabu vya Biblia,
- b. yenye mistari ya rejea chini au upandeno mwa kila Biblia,
- c. yenye itifaki nyuma ya Biblia, d. ramani chache za muhimu pia zinapatikana nyuma ya Biblia.

3. Kuwa na kalamu au penseli au kalamu ya kuweka alama (highlighter)

4. Kitabu daftari yako.

Ukiwa na vifaa hivyo hapo juu utakuwa umejizatiti vizuri tayari kwa kujifunza Biblia, na jinsi ya kufanya utafiti ukiwa thabiti kupitia Biblia. Usisite kuuliza muuzaji muuzaji kwa msaada zaidi katika kuchagua Biblia inayokufaa, na hasa katika kuchagua Biblia yenye mistari ya rejea. Hii itazungumziwa zaidi katika somo la 3.

Usisite wala kuogopa kuchora alama kwenye Biblia yako. Unaruhusiwa! Nduti maana kalamu imo kweye orodha ya vifaa muhimu wakati kusoma Biblia. Ni kitabu chako cha ku. Ifanye kuwa yako kwa kutumia notisi zako, ukipiga mistari, ukiweka alama, ikichora duara na hata kuweka miare! Pia unahimizwa kutumia kitabu chako cha kuandika kumbukumbu ili kutunza mawazo muhimu, maswali, ili kuendelea na safari yako katika kujifunza kwako.

Mambo muhimu unayopaswa kufahamu: Tafasiri mbalimbali za Biblia zinapatikana kwenye maduka ya vitabu kote nchini. Mnashauriwa kusoma Union Version, hii tafasiri imetafasiriwa toka lugha ya asiri moja kwa moja.

Kwa maandalizi haya utakuwa umejizatiti kikamilifu kwa usomaji wako na tayari kwa kujifunza kupitia maandiko kikamilifu ndani ya Biblia yako

Masomo yamegawanyika katika sehemu tano. Migawanyiko hii ni kwaajili ya kukusaidia na kukupitisha kwenye masomo kwa mpangilio na mda mda uliopangwa. Mpangilio wa mda uko mikononi mwako. Wakati mwingine somo linaweza kuhitaji muda mrefu kuliko kuliko mda ulionao, kwa hali hiyo utatakiwa kumaliza somo moja kwa kutumia kipindindi zaidi ya kimoja kufuatana na mpango wako. Wakati mwingine utaweza kumaliza somo na kuanza somo linalofuata kufuatana na mda utakao kuwa nao. Kabla ya kuanza somo la kwanza, ningetaka nikufhamishe juu ya masomo matatu ambayo yataimarisha masomo yako kuanzia mwanzoni:

1. Maneno katika kitabu hiki yaliandikwa na watu waliovuviwa na Mungu, na kuandika yale ambayo Mungu alitaka kuambia watu wake. Ukweli ulioandikwa ulikuwa ni ule ambao Mungu kusudia na kuwafunulia waandishai watakatifu. Katika somo la 2, sehemu ya 4 utapewa rejea za Biblia ambazo zitahakikisha vitu hivi:

2. Ili kuelewa kuwa Biblia vizuri zaidi tunahitaji kufahamu mambo mawili muhimu; kuwa Sheria ya Mungu na Habari Njema za Mungu ziko kwenye kitabu hiki. Mungu anatumia sheria yake kutuonyesha hali yake ya haki na maisha yetu maovu tunayoishi. Biblia inaweka wazi kuwa yale yaliyo karibi na maovu kama vile mauaji, yale yaliyokatazwa ili tuishi kwa amani katika jamii. Sheria pia huweka wazi matendo yetu maovu, kwa maneno yetu, matendo na mawazo. Mwishao sheria hutumika kama mwongozo wetu katika kufanya maamuzi na uchaguzi wa ki-Mungu na kutusaidia kufanya maamuzi mazuri.

Sheria kuuambia kuwa hatujatimiza kiwango cha Mungu. Tumepungukiwa na ukamilifu ambao Mungu anataka. Kwahiyo sheria hutuonyesha wapi tumeshindwa na Habari Njema za Mungu hutuambia jinsi Mungu anavyoshughurika na madhaifu yetu, kwa kutupatia upendo wake na masamaha kupitia Yesu Kristo. Tuna Mungu ambaye hutumia Habari njema za Yesu kufuta dhambi zetu, mashitaka na aibu maishani mwetu ambazo sheria huweka wazi.

3. Utajifunza kuwa Biblia ina Maagano mawili, Agano la Kale na Agano Jipya. Tunayojifunza katika Agano la Kale yamewekwa wazi katika Agano Jipya. Mambo ambayo hatupaswi kuyafahamu kikamilifu, huwa wazi kadiri simulizi ya Mungu inavyoendelea. Usikate tamaa iwapo baadhi ya mafundisho yataonekana kutoeleweka vizuri. Endelea kukazana na masomo yako ukiamini kuwa mwisho Mungu atasema kinachoeleweka kwako.

Mwisho inabidi uelewe kuwa masomo haya yameandikwa ili uweze kujifunza wewe mwenyewe. Yameandaliwa katika hali ambayo yatakuwa rafiki wa mtumiaji. Kwa kipimo cha nidhamu ya mtu binafsi, utaweza kusoma makala bila shida yoyote, wakati huohuo utakuwa ukifurahia masomo. Utapata ufahamu mpya na utashirikisha ufahamu huo watu wengine. Aidha utapenda kushirikisha watu wengine ufahamu wako. Pia utauliza maswali ambayo ni change moto, ambayo yatahitaji kujibiwa.

Nikitazamia mwikitio kutokana na mlivoombwa kujitahidi kukumbuka kuwaalika wanandoa marafiki zenu kusoma pamoja. Labda wewe na mwenza wako mnetaka kuwaomba wanandoa wawili au watatu kujiunga nanyi. Labda unaishi kwenye nyumba yenye uwanja wa kutosha na una marafiki ungetaka kuwaalika kujifunza nao. Labda wewe ni mshiriki wa kanisa au unafahamu kanisa ambako darasa au ukumbi umetolewa kwaajili ya wanafunzi kufanya majadiliano juu ya mambo waliyojifunza juma lililopita.

Katika mazingira yoyote yale , jenga mazingira ambayo yatawezesha kukuwezesha kukutana na kikundi kidogo mara moja kwa wiki ili kishirikishana maendeleo yao ya usomaji wa Biblia kama marafiki. Mtu mmojamoja katika kikundi chako, iwapo ni kikubwa au kidogo, ataimarisha usomaji wenu na kuendeleza ufahamu wao.

Ni wakati sasa kuwezesha safari kuanza! Fungua Biblia yako. Hebu tuanze na kichwa cha ukurasa. Ni neno gani limeandikwa kwenye ukurasa huu?

1

SOMO LA KWANZA —SEHEMU 1

Ni wakati wa kuanza. Fungua Biblia yako sehemu ya **Yaliyomo** au ukurasa uliorodheshwa kurasa zote za Vitabu vyote vya Biblia.

MAZOEZI:

Orodhesha maoni yako unapoendelea kuangalia ukurasa huu. Ukurasa huu unakuambia nini kuhusu Kitabu, Biblia Takatifu.

FUNDISHO:

1. Orodha ya vitabu imegawanyika katika maagano mawili: Agano la Kale na Agano Jipya.

➤ MAFAFANUZI:

Agano la Kale ni kundi la maandishi ya zamani, kwa asili yaliyoansikwa kwa lugha ya Kihebrania na manabii waliovuviwa na Mungu. Vitabu vitanao viliansikwa na Musa, baadhi ya vingine na manabii, na vingine viliandikwa na na wengine waliovuviwa, katika

mfumo wa mashairi kumsifu Mungu, na maelekezo ya kuishi kama Wayahudi.

Kumbuka: Mkusanyiko huu wote wa maandiko matakatifu, yanaunda msingi wa imani ya Kiyahudi.

➤ **MAFAFANUZI: Agano Jipya** is ni kundi la vitabu au maandiko matakatifu yaliyoandikwa kwa lugha ya Kiyunania na watu wa Mungu waliovuviwa. Katika Agano Jipya vimo vitabu vine vya kwanza vinavyoelezea maisha ya Yesu, kufa, na kufufuka kwake, Pia Agano Jipya inajumlisha nyaraka ishirini na zilizoandikwa na Paulo, Petro, na mitume wengine kwa watu mbalimbali wakiwamo watu binafsi na makanisa. Kitabu cha Ufunuo kanahitimisha maandiko ya Agano Jipya.

Kumbuka : Mkusanyiko wa maandiko matakatifi ya Aagano la Kale na Agano Jipya, yanaunda misingi ya imani kwaajili ya Kanisa la Kikristo.

2. Vitabu vingi viko kwenye Agano la Kale zaidi ya Agano Jipya.

Vimo vitabu vingapi katika Agano la Kale? _____

Vimo vitabu vingapi katika Agano Jipya? _____

Ni jumla ya vitabu vingapi vimo katika Biblia Takatifu?

Zaidi ya robo tatu ya vitabu vya Biblia ni Agano la Kale. Iangalie! Weka kidole kweye ukurasa, na kidole kinginge kupitia Biblia nzima na tafuta ukurasa Agano Jipya inapoanzia. Agano la Kale ina jumla ya vitabu 39 na Agano Jipya ni jumla ya vitabu 27

3. Vitabu sitini na sita vya Biblia vimeorodheshwa kushoto katika yaliyomo. Matoleo mengi ya Biblia huorodhesha vifupi vya vitabu na kurasa zake.

MAZOEZI:

Tumia orodha ya yaliyomo uandike jina la kila kitabu na kifupi chake.

ORODHA YA VITABU VYA AGANO LA KALE NA VIFUPI VYAKE (39) **(Agalia ukurasa 3)**

Somo 1 – Sehemu 1

3

Mwanzo (Mwa)

Vifupi vya Biblia

Kuifanya Biblia Iwe yako

4

MAZOEZI:

Tumia orodha ya yaliyomo na kuandika jina la kila kitabu cha na kifupi chake.

VITABU VYA AGANO JIPYA NA VIFUPI VYAKE (27)

Mathayo Mt

Vifupi vya Vitabu

4. Ukisoma majina yote kitabu kimoja kimoja utagundua kuwa kuna majina ambayo umeyazoea na mengine ni mageni. Baadha ya haya majina ni mepesi kutamkika na mengine ni changamoto katika kuyatamka. Unaweza kufanya mazoezi kwa kutamka majina ambayo ni changamoto kwako kwa sauti. Itakufurahisha kugundua kuwa orodha haikatishi tama kama invyoonekana mwanzoni. Endelea kujaribu mara nyingi ukifanya mazoezi!

5. Majina mengi ya Biblia yamekuwa ya kawaida kwetu, kwasababu baadhi ya wazazi wamewaita majina hayo watoto wao. Inawezekana jina mojawapo ni lako. Tumia mda kunakili orodha orodha ya majina yale unayoyafahamu kati ya majina ya Biblia, kwenye daftari yako.

SOMO LA KWANZA — SEHEMU 2

ZANA #1:

Kati kusoma Biblia yote **Sura na mistari** iliwekwa. Sura na mistari haikuwapo katika misaafu ya kwanza ya maandiko, ila iliwekwa na wasomi kama njia iliyokubalika kwaajili ya kuonyesha rejea na nukuu kwa wakati fulani.

MAFUNDISHO:

Tutatumia sura ya kwanza ya kitabu cha Mwanzo kama kielelezo katika kujifunza. Fungua kwenye ukurasa unaoonyesha jina la kitabu cha Mwanzo. Ukurasa wa jina, unatapatikana kwenye Yaliyomo. Kitabu kimeanza na namba “1”. Namba hii kubwa, inaashiria kuanza kwa sura.

➤ **MAFAFANUZI:** Sura ni sehemu kubwa ya kifungu au maandiko matakatifu, ambayo yana mistari mbalimbali.

Kumbuka: Kitabu cha Biblia kinweza kuwa na sura moja, kv. Filemoni au Yuda, wakati vitabu vingine vinaweza kuwa na sura sura nyingi kama therathini au zaidi, mfano Isaya au Yereimia.

Ukiangalia kwa karibu utagundua kuwa kuna namba ndogo zimeandikwa katikati ya kifungu cha maandiko. Namba ndogo “1” inaweza isiwepo kwasababu inaaminika kuwa ipo pasipo kuandikwa. Angalia namba 2 ndogo. Hii namba ndogo inaonyesha mstari.

➤ **MAFAFANUZI:** Mstari una maneno au sentensi. Muunganiko wa mistari mbalimbali hutengeneza sura.

Kumbuka: Mistari hutofautiana katika urefu. Mistari iliyo mifupi zaidi ya mingine ni Yoh. 11:35. “Yesu akalia machozi”na Ayu 3:2, “Ayubu akajibu na kusema”. Mstari ulio mrefu zaidi ni Esta 8:9 Angalia mstari huu mwenyewe! Ni maneno mangapi yako kwenye mstari huu?-----

Katika mazoezi inawezekana ukatakiwa kuangalia baadhi ya vifungu. Maelekezo yanapaswa kujumlisha orodha ya sura na mistari ndani ya kitabu husika cha Biblia ambamo vifungu hivi na rejea, zinapaswa kuonekana.

➤ **MAFAFANUZI:** *Kifungu au rejea* kinaweza kuwa mstari, baadhi ya mistari, sura, au sura tofauti katika Biblia.

Kama ilivyofafanuliwa, mistari tofauti hutengeneza sura. Inapoonyesha rejea ya mstari wa pili wa sura ya Mwanzo, mtu anapaswa kuitaja kama Mwanzo sura ya 1 na mstari wa 2, au Mwanzo 1 mstari 2. Pomoja na ukweli huo, katika kuandika, maneno yanaandikwa kwa mfumo wa ufupisho: Mwanzo 1:2. Alama ya kutaja hutenganisha sura na mstari. Kwa kutumia ufupishao itaonekana hivi: Mwa. 1:2. Chukua mda mfupi kuangalia rejea hizi katika Mwanzo. Kuhakikisha kuwa umepata Mwa. 1:2, mstari unaanza na maneno, “Nayo nchi ilikuwa ukiwa....”

MAZOEZI:

Hebu tufanye mazoezi. Kuwa na uhakika wa kutumia orodha ya Vitabua vya Biblia, vinavyopatikana kwenye sehemu ya yaliyomo, kama huna uhakika wapi kitabu kinapatikana. Sasa twende! Angalia hii mistari ya rejea na uandike neno la kwanza au sentensi.

• Mwanzo 22:13 – mstari unaanza,
“

”

• Kutoka 14:13 –mstari unaanza,
“

”

• Mathayo 5:13 – mstari unaanza,
“

”

Ulifanyaje? Kama ulifanikiwa majibu yako yatasomeka:

- Mwanzo 22:13 - “Abraham akainua macho yake akangalia, na tazama kondoo.....”
- Mwanzo 14:13 - “Musa akawaambia watu, msiogope.....”
- Mathayo 5:13 - “aNinyi ni chumvi ya dunia.....”

Unaweza kuchukua mda mwingine mfupi wa kufanya mazoezi zaidi, lakini sasa umejizatiti na zana ya kukusaidia kusomo Biblia, ili iweze kukusaidia katika kukua kwako kiroho na kuzidi kujifunza.

SOMO LA KWANZA —SEHEMU 3

MAFUNDISHO:

Vitabu vya Biblia viko kwenye mpangilio; pamoja na hayo, mpangilio huo hauko kwenye mtiririko wa kufuatana. Katika sehemu ya sehemu ya 3 tutaona mpangilio wa vitabu vya Agano la Kale, na baada ya hapo tutarudi kwenye vitabu vya Agano Jipya.

Vitabu vya Agano la Kale vimepangiliwa katika makundi manne. Unaweza kuweka alama kwenye makundi ya vitabu hivi katika yaliyomo kwenye Biblia yako.

Kundi 1: Vitabu vya Torati au vitabu vya *Sheria*. Vitabu hivi ni vitabu vitano vya kwanza vya Biblia, na viliandikwa na nabii Musa. Mara nyingine vinajulikana kama vitabu vya Musa. Walimu wa Kiyahudi wanaweza kuviita *Torati*.

Vitabu hivi vya sheria vina sheria zote za Kiyahudi, mafundisho, na maelekezo kwaajili ya utaratibu wa maisha kama taifa la Israel. Vitabu hivi vimetengeneza mila na tamaduni za watu wa Israel. Vitabu vya sheria hujumuisha vitabu vifuatavyo:

- a. Mwanzo d. Hesabu
- b. Kutoka e. Kumbukumbu la Tarati
- c. Mambo ya Walawi

MAZOEZI:

Sasa hebu tuchunguze mfano wa maelekezo *kwa utaratibu wa maisha ya Wayahudi* yanayopatikana kwenye vitabu vya sheria. Tafuta Kutoka 12. Mistari ishirini na nane ya kwanza, inazungumza juu ya Pasaka. Katika

mistari 14 – 20 Mungu anatoa maelekezo maalum kwaajili ya watu wake, Waisrael. Soma haya maelekezo. Ni yapi maelekezo yake mengine? Umegundua nini?

- _____
- _____
- _____
- _____

Lengo la zoezi hili si kwaajili ya kuelewa mambo yote, na si kwaaji ya kufikiria sana matukio yaliyo kwenye simulizi. Zoezi hili, limekusudiwa kuwa mfano wa mila ambayo Mungu alianza kwaajili ya watu wake. Mungu aliwapa wana wa Israel maelekezo kwa uangalifu kuhusiana na Pasaka, Aliwataka wakumbuke milele usiku alipopita nyumba za wana wa Israel lakini akawapiga wazaliwa wa kwanza wa Misri. Chakula hiki kiliitwa chakula cha Pasaka, ikikumbusha usiku wa wana wa Israel. Somo hili linagusa na lina mafundisho ya muhimu.!

Kundi 2: Vitabu vya Historia: Kundi lingine muhimu lina vitabu ambavyo vina kumbukumbu ya historia ya taifa la Israel. Vitabu vya Historia ni:

- a. Yoshua
- b. Waamuzi
- c. Ruthi
- d. Samwel cha Kwanza na cha Pili
- e. Wafalme wa Kwanza na cha Pili
- f. Mambo ya Nyakati cha Kwanza na cha Pili
- g. Ezra
- h. Nehemia
- i. Esta

MAZOEZI:

Hebu tuangalie katika historia, kwenye matukio ya kihistoria katika moja ya vya Historia, Kitabu cha Yoshua. Inawezekana iwe hujawahi

kusikia simulizi hii. Furahia kusoma simulizi ya matukio katika Yoshua

6. Kumbuka maswali haya:

1. Tukio hili lilitokea wapi?

___ (mstari 1)

2. Nani alikuwa muhusika mkuu?

___ (mstari 2)

3. Mungu alifanya nini?

___ (mstari 20)

Somo la 1 Sehemu ya 3

MATUMIZI:

Israel walikuwa na kuta za kushinda. Ni upi ambao unaweza kuwa ukuta wako unao kusumbua hadi sasa? Ni wapi umeshuhudia Mungu akifanya kazi akiangusha ukuta katika maisha yako?

MAOMBI:

Bwana Mungu, nakushukuru kwa kufanya kazi katika maisha yangu kuharibu kuta ambazo zilitishia kunitenga na wewe. Amen.

SOMO LA KWANZA —EHEMU 4

FUNDISHO: (Kusonga mbele!) Kuweka vitabu vya Agano la Kale katika makundi.

Kundi 3:**Vitabu vya Mashairi.** Vitabu hivi vinajumuisha mashairi, nyimbo, na maandiko ambayo yanajulikana kama maandiko ya hekima. Vitabu vya Mashairi hujumuisha:

- a. Ayubu, ambacho hufahamika kama kitabu cha zamani zaidi ya vitabi vyote vya Biblia
- b. Zaburi
- c. Methari
- d. Mhubiri
- e. Wimbo uliobora, ambacho hufahamika kama Wimbo wa Sulemani.

MAZOEZI:

Mhubiri 3:1-8 ni mfano . Soma mistari hii na uone kama imezoeleka kwako. Mstari mwingine kutoka ushairi ni kutoka Zab. 23. Soma Zaburi. “

- Andika mistari wa kwanza.
-

- Sasa soma mistari mingine. Ni mistari gani katika Zaburi hii una maana fulani kwako?
-

- Kwanini huu ni mistari wa pekee kwako?
-

Kuifanya Biblia Iwe Yako

MAOMBI:

Asante Bwana Mungu, kwa kuwa mchungaji wangu. Asante kwa kunitunza na wale ninao wapenda. Amen.

Kundi 4: Vitabu vya Manabii. Vitabu vilivyo andikwa na Manabii vimegawanyika makundi mawili. *Manabii wakubwa na Manabii wadogo.* Manabii walichaguliwa na Mungu na waliitwa na Mungu ili waseme Neno lake kwa watu wa Israel.

Vitabu vinne kujumrisha na Kitabu cha Maombolezo, ambacho nacho pia kiliandikwa na Yeremia, kinachukuliwa kama vikubwa kutokana na urefu wa vitabu hivyo. Maandiko ya manabii wakubwa ni makubwa mara tatu zaidi ya manabii wadogo. Kwasababu Mungu alitaka uhusiano wa karibu na wana wa Israel ambao aliwachagua kuwa watu wake. Aliwapa manabii kazi ya kuwapa:

- 1)Neno la hukumu kwao kutokana na maisha ya uovu waliyoamua kuishi.
- 2)Wito wa kugeuka kutoka kwenye njia ya uovu waliyochagua, na
- 3)Ahadi ya rehema na urejesho wa uhusiano na wote waliogeuka nyuma wakamuacha. Mara nyingi katika mda tofauti walielekezwa kwa yule ambaye Mungu angemtuma Mkombozi wa tofauti na wa pekee .

Manabii wakubwa hujumuisha:

- a. Isaia c. Ezekieli
- b. Yeremia (na Maombolezo) d. Danieli

MAZOEZI:

Vifungu vifuatavyo hutoa mifano mitatu ya *kazi ya manabii*, Onyesha kifungu ambacho huzungumzia *hukumu*, vifungu ambavyo huita Israel kugeuka na *kurudi* kwa Bwana Mungu, na kifungu ambacho huongelea ahadi ya Mungu, na kile ambacho huonyesha ukombozi wa karibu wa Mungu. Andika kifungu cha maneno kutoka kwenye mistari hii ambayo hubainisha hukumu, wito wa kurudi, ahadi na tumaini la ukombozi wa Mungu kwa wanadamu.

1. Yeremia 4:16-18
-

2. Yeremia 4:1-4
-

Somo la 1 Sehemu ya 4

3. Yereimia 29:11

4. Yereimia 23:5-6

MATUMIZI:

Katika kifungu hiki cha tatu, Yereimia amawakubusha wana wa Israel kwamba Mungu huwajali, na anataka kuwapa matumaini ya nyakati zijazo. Ahadi zinazofanana na hizo ni zangu na zako pia. Anapenda kutupa matumaini siku zijazo. Tukijua na kuamini kuwa ahadi Yake ni ya kweli kwako, hii inaweza kuleta tofauti gani katika maisha yako ya sasa?

MAZOEZI:

Simulizi ya kisanaa inaonekana katika kitabu kingine cha *Unabii mkubwa*, kitabu cha Daniel. Soma Danieli 3

- Ni aki na nani wahusika maalum? (mstari 12)

_____,
_____, na

- Ni yapi yaliyowapata? (mistari 19-23)

- Ni kwanini walipatwa na haya yote? (mistari 13-15)

MATUMIZI:

Maisha yanaweza kuwa magumu wakati fulani, na tunaweza kujisikia wapweke. Habari hii inatuhakikishia kuwa “Mungu tunaye mtumikia yuko tayari kutuokoa.....”. (Danieli 3:17)

SALA:

Asante Bwana, kwa kunipenda na kunihakikishia kuwa uko pamoja namo kama ulivyokuwa na Shedraki, Meshaki na Anedinego. Uko pamoja nami hata wakati ninapokosa matumaini na kujisikia mpweke. Asante Yesu, Unanipa tumaini kwa maisha yajayo, nikiwa pamoja nawe milele. Amen.

SOMO LA KWANZA —EHEMU 5

FUNDISHO:

Bado zaidi... Kundi la 4. **Vitabu vya Manabii** endelea na *manabii wadogo* vitabu kumi na viwilli ambavyo hujumuisha:

- a. Hosea e. Yona i. Sefania
- b. Yoel f. Mika j. Hagai
- c. Amosi g. Nahumu k. Zakaaria
- d. Obadia h. Habakuki l. Malaki

MAZOEZI:

Simulizi unayoweza kutambua, ni habari za Yona; samaki mkubwa. Chukua mda wa kujisomea sura nne za kitabu cha Yona. Kwa kutafakari soma sala yake akiwa ndani ya samaki katika sura ya 2.

MASWALI:

1. Muhusika mkuu ni nani kwenye simulizi hii?

2. Alikabiriwa na nini?

MATUMIZI:

1. Uliish ingia kwenye mazingira ambayo yalikufanya ujisikie kama Yona alivyojsikia?

16

2. Mambo yalikugeukaje?

3. Andika kwenye daftari yako baadhi ya fikra zako na maelezo juu ya hisia yako.

SALA:

Bwana Yesu, wakati mwingine hujisikia kana kwamba niko ndani ya samaki japokuwa ninaishi, lakini unanijia na kunitia matumaini na kunitia moyo. Unaniokoa ili niweze kuishi tena. Asante. Amen.

SOMO LA PILI —EHEMU 1

UTANGULIZI:

Katika somo la 1, tulianza na kuelezea maneno kama vile sura na mistari, na tuliangalia mpangilio wa vitabu vya Biblia vya Agano la kale. Hii ni kumbukumbu wakati tukiendelea na mpangilio wa vitabu vya Agano Jipya. Inawezekana umeisha anza kujiuliza maswali,

maswali mengi!. Hilo ni jambo jema. Uwe na uhakika wa kuyaandika nje ya mstari wa majini wa masomo yako au ndani ya daftari yako.

Unatiwa moyo kuuliza maswali, lakini uangalie yasisije yakawa kigingi cha njiani katika kujifunza kwako. Majibu mengi yatasawazisha kadiri unavyoendelea na kujifunza, na unavyo endele kushirikiana na wengine katika majadiliano.

FUNDISHO:

Agano Jipya pia limepangwa katika makundi manne. Wakati ukiendelea kujifunza tofauti ya makundi haya unaweza kuweka alama kwenye orodha ya yaliyomo ili uweze kuyatofautisha.

1. **Injili:** Hivi ni vitabu vinne vya kwanza vya Vitabu vya Agano Jipya.

➤ MAFAFANUZI:

Neno **Injilil** lina maana ya Habari Njema.

Kumbuka: Injili huelezea Habari Njema za upendo wa Mungu kwa wanadamu. Inili huelezea Habari Njema za Yesu.

Waandishi wa Injili huelezea simulizi za Yesu – Maisha yake, kufa kwake, na kufufuka kwake, Zinatuambia Habari Njema kuwa dhambi zetu zimesamehewa. Kutokana ba kifo cha Yesu na kufufuka kwake, uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu umerejeshwa. Kila mmoja wa waandishi wanne wa Injili uelezea ushuhuda wa kujionea kwa macho , na pia mitazamo tofauti kati ya misingi inayofanana.

Vitabu vya Injili ni:

- a. Mathayo c. Luka
- b. Marko d. Yohana

MAZOEZI:

Kwa kutumia Injili nne, soma mistari ya rejea na uonyeshe Hahari njema kwa kila kifungu.

- Mathayo 5:7 – Habari njema ni
-
-

- Marko 2:1-5 – Habari Njema ni
-
-

- Luka 15:3-7 – Habari njema ni
-
-

- Yohana 8:31-32 – Habari Njema ni
-
-

2.**Matendo** kiliandikwa na Mtakatifu Luka, mwandishi wa Injili. (Angalia Mdo 1:1). Kwa kawaida kitabu hiki kinajulikana kama *Matendo* na wakati mwingine kama *Matendo ya Roho Mtakatifu*, au *Matendo ya Mitume*. Hii kumbukumbu ya historia, hutupatia taaria za Kanisa la kwanza kama lilivyoanzishwa Yerusalemu, na baadae likaenea dunia nzima. Maono ya Mungu kuhusu Kanisa, yalifafanuliwa na Yesu kwa wanafunzi wake kabla ya kupaa kwake mbinguni.

MAZOEZI:

Soma Mdo 1:8, na kumbuka kupitia malengo haya ukuaji wa kanisa na jinsi lilivyoenea kupitia eneo la Uyahudi likianza Yerusalemu kama kitovu, na hatimaye dunia nzima.

SOMO LA PILI —SEHEMU 2

FUNDISHO:

2. **Nyaraka:** Vitabu Ishirini na moja (21) ni nyaraka
3. ➤ **MAFAFANUZI:***Nyaraka* ni barua. *Kumbuka: Paulo aliandika Nyaraka zilizo nyingi.*

Petro, Yakobo, na Yohana ni baadhi waandishi wengine.

Hizi nyaraka ziliandikwa kwa makusudi ya kutia moyo na kuimarisha makanisa yaliyokuwa yameanzishwa kote ulimwenguni , na watu wanao tajwa. Nyaraka hizo ni:

- a. Warumi
- b. 1 &2 Wakorintho
- c. Wagalatia
- d. Waefeso
- e. Wagalatia
- f. Wakolosai
- g. 1& 2 Wathesalonike
- h. 1 & 2 Timotheo
- i. Tito
- j. Filemoni
- k. Wahebrania
- l. Yakobo
- m. 1 & 2 Petro
- n. 1, 2 & 3Yohana
- o. Yuda

MAZOEZI:

Mfano wa maneno yaliyoandikwa kutia moyo na kuimarisha kanisa ni: Wafilipi 4:6. Huu ni mstari wenye wa maneno yenye nguvu na ya kutia moyo kwa wakristo waliokuwa wakiishi kwa hofu, ukiwatia moyo kuvumilia mateso, na hata kufa chini ya mtesaji ya mtawala aliyeitwa Nero.

Andika maneno yaliyo kwenye mstari wa 6:

MATUMIZI:

Ni yapi baadhi ya mambo ambayo hunifanya kuwa na mahangaiko ya maisha? _____

Mungu hakukusudia tuwe waoga au kusumbukia maisha. Je anatumiza tufanye nini wakati tunapojisikia kusumbukia maisha au kukata tama?
?

Je Mungu anaahidi nini katika mstari wa 7?

SALA:

Bwana Mungu, asante kwa kunijali na mahangaiko ninayo beba moyoni. Nipe moyo wa shukrani ambao una nikumbusha jinsi unavyo nipatia mahitaji yangu kwa wakati uliopita na utaendelea kufanya hivyo siku zijazo. Asante kwa kuniahidi amani ambayo huja kwa kumjua Yesu kama Bwana na Mwokozi wangu. Amen.

SOMO LA 2 SEHEMU YA 2

4. Apokrifa:

Kitabu cha Ufunuo ni kitabu pekee katika Agano Jipya kinachoitwa maandiko ya apokrifa.

➤ **MAFAFANUZI: Maandiko ya Apokrifa** Neno apokrifa lina maana ya “kufunua” au “kudhihirisha”. Maandiko ya Apokrifa ni taswira au lugha ya picha ambayo hukusudia kufunu au kuweka wazi siri za ulimwengu wa kimbingu.

Kumbuka: Ufunuo iliandikwa na Yohana. Ilikuwa ni kumbukumbu ya maono ya kiunabii iliyoandikwa na Yohana alipokuwa mfungwa kizuizini

MAZOEZI:

• Yohana aliishi kizuizini ? (Ufunuo wa Yohana 1:9)?

• Tumia muda kusoma sehemu ya sura ya 15.

Sura hii itakupatia hisia ya lugha ya picha ambayo inadai kutumia ubunifu wetu kuelewa.

Ni picha gani inayoshauriwa katika Ufunuo wa Yohana 15:1-2?

1.

2.

3.

SOMO LA PILI — SEHEMU 3

FUNDISHO:

Mbinu za uandishi za waandishi tofauti hutofautiana. Mtu mmoja mmoja alitumia njia tofauti kuwasilisha Neno la Mungu kwa watu. Koramu upande wa kushoto inatoa mbinu sita tofauti. Kolamu inayofuata, rejea za ki-Biblia, zinaonyesha wapi unaweza kuona mfano wa mbinu maalumu. Kolamu ya tatu imekusudia kukupatia ufahamu wa baadhi ya ufahamu wa rejea na kolamu ya mwisho inakupa nafasi kwaajili ya maswali yako mwenyewe au maoni yako, ambayo yanaweza kutokana na masomo yako.

MAZOEZI:

Rejea za ki-Biblia

Maoni

Maswali yako, maoni

Maelezo

Mathayo 4:18-22

Mistari hii hutoa simulizi za Yesu akiita wanafunzi wake watatu.

Ushairi

Zaburi 8:1-9

Waandishi walitumia ushairi kuongelea

utukufu wa Mungu

kama muumbaji na uhusiano wake na mwanadamu aliyemuumba.

Mithali

Mithali 11:25

Kinacho semwa ni nini kwenye sehemu ya kwanza

Kwa kawaida mstari wa kwanza wa methari

huwa inaanza tena ili ieleweke katika sehemu ya pili.

Unabii

Isaia 9:6

Unabii siyo kubahatisha
badala yake ni kueleza mambo yajayo
Unabii huu husema mtomto atazaliwa

mifano

(angalia ukurasa unaofuata)

Luka 18:9-14

Ukweli wa kiroho: “Ajikwezaye
atahushwa, na ajishushaye atakwezwa”

Apocalyptic Vitabu vya apokrifa

Ufunuo wa Yohana 6:1, 2

Hii mistari huzungumzia

dubu, viumbe hai, a

Faraso mweupe na mpanda farasi wake,

Katika lugha yote ya ki apokrifa

➤ **MAFAFANUZI:**

Mfano inaeleweka kama hadithi ya duniani yenye maana ya kimbinguni.

Kumbuka: Kwa asili jamii ya kiyahudi ilizungumza katika mifano au hadithi kufundisha.

Yesu alitumia kile kitu ambacho watu walijua, na mara nyingi alitumia lugha ambayo ingeeleweka kuhusiana na mambo yanayohusu Mungu. Angetumia mazingira na nafasi iliyokuwapo, ili iweze kuendana na maisha ya kila siku, mfano kupanda mbegu, shilingi iliyopotea, mwana mpotevu, au kupokea mshahara kwa ajira. Mifano kawaida hutoa maadili au ukweli wa kiroho.

mtoto mkaidi, au kupokea mshara kwa kuajiriwa. Mfano kawaida hutoa maadili au ukweli fulani ea kiroho.

SOMO LA PILI — SEHEMU 4

MAFUNDISHO:

Maswali na majibu ni sehemu na maana halisi ya kusoma Neno la Mungu. Mara nyingine tunauliza maswali kwasababu tunahitaji kuchimba zaidi na kupata elimu zaidi na ufahamu. Na mara nyingine tunauliza maswali kwasababu hatuelewi. Na pia tunauliza maswali kwasababu ya hali halisi katika maisha ambayo hayakubaliani ba mafundisho ya Neno la Mungu.

Kama tulivyosema katika utangulizi wa somo 2-sehemu1, ni vizuri kuuliza maswali. Maswali huruhusu Roho wa Mungu kufanya kazi ndani yetu, kama Asemavyo katika mioyo yetu na mawazo, akituelekeza kwenye kiwango cha uelewa wa Mungu ni nani na uhusiano anaotaka tufurahi pamoja naye.

Kwa wakati huohuo, ni muhimu kwetu tukubali kwamba siyo maswali yote yenye majibu. Baadhi ya maswali yanahitaji utafiti wa ukweli. Maswali mengine yanahitaji subira kwa imani kwamba kwa wakati uliokubalika ufahamu wa ndani na uelewa vitapatana na majibu yanapatikana. Pamoja na hayo, maswali mengine hubakia kuwa maswali. Sisi ni wanadamu wenye mwili wenye mipaka ya ufahamu. Mungu hana mipaka ana ufahamu wote, ambao ufahamu wetu hauweze kuelewa. Maswali yote yanaweza kuibuliwa na majibu yake kutafutwa baadae.

Lakini izingatiwe kuwa, si maswali yote yatakuwa na majibu. Inatupasa kumwangalia Mungu kwa imani tukiamini kuwa Anafahamu mambo yote. Anajua na anatutakia yaliyo mema. Utagundua katika somo hili kuwa kila swali lina nafasi iliyotolewa kwaajili ya majibu. Aidha inatupasa kufahamu kwa kila swali kuna swali la matumizi ya nyongeza. Swali la matumizo lilifafanuliwa katika Somo 1, lakini masomo yanakupeleka kwenye ufahamu mpya wa maswali ya kimataifa.

Kadiri unavyoendelea kujifunza Neno la Mungu, ni muhimu kuangalia umuhimu wa kuunganishwa kwenye lile ambalo Mungu alilifunua kwa watu miaka mingi iliyopita, na kufahamu lile asemalo maishani mwangu katika karne ya 21. Mungu habadilishi mawazo yake. Yale aliyoyasema miaka mingi iliyopita anayasema na sasa. Malaki 3:6 “Kwakuwa mimi Bwana sina kigeugeu”.

Ukiendelea kuangalia uhusiano, utanza kuuliza maswali. Swali linawezekana likawa:

Kuna kipimo gani kipya ambacho Neno la Mungu linacho kwaajili yangu kadiri ninavyoendelea kufanyia kazi mafundisho katika mahusiano tofauti, matukio tofauti na kwa watu ninao kutana nao siku kwa siku?

Maswali ya matumizi hutafuta majibu kwa “ili iweje?”. Kwa maneno mengine, Maswali ya matumizi hutafuta majibu ya kwa ya “ili iweje?” Kwa maana nyingine, kama ndivyo Mungu asemavyo, *ili iweje*, hii ina maana yoyote katika maisha yangu? Maswali ya matumizi husaidia Maswali ya matumizi hutafuta majibu ya “ili iweje?” Kwa maana nyingine ni, kama Mungu asemavyo, *ili iweje* ina maana gani kwangu na maisha yangu?

Maswali ya matumizi huangalia ni wapi Neno la Mungu huendana na maisha yetu. Maswali ya matumizi ni rafiki wa karibu na tafakari ya ndani ya nafsi katika hali ya kawaida ya maisha yetu. Mara nyingine nikukumbushe kuwa ili iweze kuendeleza safari yako hii ya masomo, uwe na uhakika wa kuandika itikio lako la maswali ya kutafakari kwenye daftari yako, au ndani ya mstari wa majini wa kitabu chako cha masomo.

_____,
_____,
_____.

na _____

Somo la 2 Sehemu ya 4

27

Temotheo 3:17 – “ili mtu wa Mungu
aweze _____

MATUMIZI:

- Je huwa ninafikiri kuwa Neno la Mungu ni la msaada kwangu.? (2 Temotheo 3:16)?

- HNinaweza kuingizaje Neno la Mungu kwenye kuchangua kwangu na kuamua kwangu wakati nikiwa nyumbani na familia yangu, mahali pa kazi,na jamii kwa ujumla?

SALA:

Bwana Mungu, asante kwa wale waliokuwa watiifu kwako na kuandika walioandika Neno lako la kweli. Fungua moyo wangu nikusikilize Wewe, ongea nami ninapoendelea kusoma na kujifunza Neno Lako. Nisaidie niingize neno lako kwenye maisha yangu. Fungua macho ya moyo wangu nione jinsi upendo wako ulivyo mwingi.

Amen.

SOMO LA PILI — SEHEMU YA 5

MAFUNDISHO:

Tulianza na yaliyomo kutufahamisha vitabu tofauti vinavyounda Biblia. Sura na mistari vilikuwa ni vitu vya kwanza vya kutembelea. Zana hizi zinakuwezesha wewe kama mwanafunzi kuwa tayari kufungua rejea za Maandiko kwaajili ya kusoma. Zana za nyonge zinapatikana kwa baadhi ya Biblia lakini siyo zote. Zana hizi ni: 1) Ramani za sehemu zilizotajwa na waandishi kwenye vifungu, 2) mistari ya rejea, na 3) itifaki. Hizi zana zinatolewa ili kukusaidia kuwa mzoefu zaidi wa Biblia kama kitabu, na kukuwezesha katika kujifunza kwako. Katika somo hili utafahamishwa juu ya ramani mbalimbali kama zana. Kwenye masomo yanayofuata, utapata nafasi ya kuelewa mistari ya rejea na itifaki.

ZANA #2:

Kuanza kujifunza Zana #2 unaelekezwa kuonyesha Israel ya sasa kwenye ramani. Ungawa mipaka ya nchi imebadirika kwa namna fulani, utakumbushwa jinsi ilivyo ndogo na jinsi ilivyo kwenye mazingira ya hatari, ikilinganishwa na nchi kama Misri, Uturukik, na Saudi Arabia. Nchi ya Kanaani, Israel ya sasa, ilitolewa na Mungu kwa Israel, lakini wana wa Irael iliwabidi wapigane vita wakiwa chini ya uongozi wa Yoshua, mrithi wa Musa, ili kumiliki nchi hiyo. Kwa kawaida **ramani** huwekwa mwishoni mwa Biblia. Kwenye baadhi ya Biblia huwa zina mafafanuzi kuhusu ramani. Pamoja na hayo, kwenye Biblia zilizo nyingi

ramani ni msaada kwa sehemu tu, wakati mwingine hutoa maelezo yasiyo ya kutosha.

Kwenye orodha ya ramani zinazofuata, zinaonyesha miji na majimbo, yanayofanana na vipindi au nyakati tofauti katika historia ya Biblia. Mistari ya rejea iliyoorodheshwa hapa chini itakuelekeza kwenye mistari husika. Fungua kwenye ramani kwenye Biblia yako, anza kujizoesha na mataifa ambayo hujazoea. Anza kutumia ramani kama zana katika kujifunza kwako:

- Ramani 1: Dunia ambayo wahusika wa kwanza wa kitabu cha kwanza cha Biblia yaani Mwanzo, waliyo yafahamu. Rejea: Mwa.

12:5 – Mahali pa Huru, mji wa Abrahamu aliouacha alipoelekea Canaani.

- Ramani 2: Jangwa ambalo wana wa Israel walitembea. Rejea: Kut. 16:1

Elimu, mji ambao wana wa Israel waliacha, na jangwa walikokwenda, Jangwa la Sinai.

- Ramani 3: Nchi ambayo ilikuwa mali ya kila kabila la Israel. Rejea: Yoshua 19:1-9 –

Onyesha nchi waliyokuwa wamepewa kabila la Simeoni.

- Ramani 4: Nchi ambayo ilikuwa imetawaliwa na mfalme wa kwanza wa Israel: Sauli, Daudi na Sulemani Rejea: 2 Samweli 2:1 – Mahali ilipo Hebroni, karibu na Yerusalemu.

- Ramani 5: Miji na majimbo ambayo Yesu alitembelea. Rejea: Luka 2:4 – Onyesha Bwawa la Sulemani ndani ya Yerusalemu.

- Ramani 6: Eneo la Yerusalemu wakati wa Yesu. Rejea Yohana 9:7: – Onyesha eneo la Nazareti na Beterehemu.

- Ramani 7: Ramani ya mchoro wa jimbo katika ziara ya tatu ya Mtakatifu Paulo. Rejea: Acts 16:1 – Onyesha Listra na Deba kati Galatia. Usishughurike na miji yote, majina, au maelezo kuhusu ramani. Badala yake jitahidi kuzifahamu vizuri ramani zinazopatikana na ufahamu mahali pa kuzipata.

Kila ramani imetengenezwa kusaidia kutembea vizuri kwenye safari yako kupitia nchi ya Israeli na nchi zinazopakana nayo.

SOMO LA TATU — SEHEMU 1.

ZANA #3:

Mistari ya rejea – Mistari ya rejea kwa kawaida zinapatikana kwenye kolamu ya chini, au upandeni kufuatana na chaguo la mchapaji. Katika baadhi ya Biblia hasa za Lugha ya Kingereza, mistari ya rejea sura na mistari, herufi zake zimeandikwa kwa wino uliokolezwa.

MAZOEZI:

Hebu tujaribu mifano. Fungua Mwanzo 1. Chunguza kolamu ya mistari ya rejea chini au upandeni mwa kolamu kwa kila ukurasa.

Sasa soma maneno matatu ya kwanza kwenye mstari wa kwanza wa sura ya 1: “Hapo mwanzo....”. Baada ya neno “mwanzo” utakuta herufi ndogo “a”. Nenda kwenye kolamu ya mstari wa rejea. Tafuta rejea yenye maneno ya kukoleza inayosoma 1:1, ikionyesha Mwanzo sura 1, mstari 1. “a” ndogo itakuwa na orodha za rejea tano au sita tofauti. Idadi ya rejea inaweza kutofautiana kati ya tafsiri moja na nyingine. Tafadhari zingatia kuwa japo idadi za rejea zinaweza kutofautiana kufuatana na tafsiri au lugha, au toleo na toleo, lakini Biblia za tolea lilelile hufanana. Union version zote zinakuwa na rejea zinazofanana. Mwanzo. 1:1 itakuwa inafanana kwa kila Biblia ya Union version.

Mistari ya rejea iliyoorodheshwa “a” katika Mwanzo 1:1 inaweza kujumuisha Zaburi 102:25 na Yohana 1:1-2. Onyesha rejea kwenye kolamu za rejea. Utaona kuwa kila mstari una sentensi “hapo mwanzo”.

- Mwanzo 1:1 inatwambia kuwa “*hapo mwanzo* Mungu aliumba mbingu na nchi”
- Zaburi 102:25 inasema “*hapo mwanzo*” wewe [Mungu] aliweka misingi ya dunia....”

- Yohana 1:1-2 pia anatuambia “*hapo mwanzo*” kulikuwa Neno, na Neno lilikuwa na Mungu, na Neno lilikuwa Mungu, na Neno alikuwa Mungu. Alikuwa na Mungu hapo mwanzo”

SOMO LA TATU — SEHEMU 2

MAFUNDISHO:

Mistari ya rejea huthibitisha na kusisitiza ukweli. Kimsingi, rejea zote tatu huthibitisha ukweli kwamba *hapo mwanzo* Mungu aliumba mbingu na nchi. Mistari ya rejea pia hutusaidia kufaidi ya karibu katika ukweli wa ndani kadiri Mungu anavyojifunua kwetu. Yohana 1:1-2 huthibitisha ukweli kuwa *hapo mwanzo* Mungu aliumba mbingu na nchi, lakini hutuongoza kuamini kwamba kuna zaidi! Hebu tuendeleo. Mungu ni Mungu wa mahusiano, na anataka tukue katika mahusiano yetu na Yeye. Tuna mahusiano na watu mbalimbali katika maisha yetu. Kuendeleza mahusiano kwa kina zaidi, kwa mafanikio zaidi, kwa kiwango cha juu zaidi na kwa uelewa zaidi.

Tukirudi nyuma kwa Yohana 1:1-2. Katika mistari hii, Yohana anataja kwamba, “*hapo mwanzo* kulikuwa na Neno”

Hiyo inaibua swali: Dunia ilikuwa ni nini iliyokuwapo *hapo mwanzo*? Mistari 2 unanza swali linguine: Hili ndilo Neno lililokuwa na Mungu *hapo mwanzo* akiwa kama Mungu, ambaye *hapo mwanzo* aliumba mbingu na nchi wa Mwanzo1:1? Kumbuka kwamba, kwenda kwa kina huibua maswali. Usijishughulishie na majibu kwa sasa hivi, ila endelea kuuliza na kuyaweka kwaajili ya kipindi kijacho.

Neno la kutia moyo:

- Usisite kutumia sehemu ya yaliyomo ya Biblia yako kwaajili ya kujifunza vifupi. Utaanza kuvikumbuka kadri unavyoendelea kuvitumia.
- Mistari ya rejea imeandaliwa kuwa zana ya kukusaidia, isikuchanganye. Utaendeleza kwa kutumia mistari ya rejea ukiendelea kukua katika kujifunza kwako. Kujifunza jambo jipya unaloanza kujifunza, lisiwe kikwanzo cha kukufanya usiendeleo mbele.

• Kadiri unavyoendelea kutumia zana hii utajikuta ukisafiri toka hatua moja ya maandiko kwenda nyingine. Tumia daftari yako kuongoza safari yako kutunza kumbukumbu ya uvumbuzi unaokutana nao katika sehemu tofauti. Katika hatua za kusafiri utanufaika kwa kupata ufahamu zaidi jinsi Agano la Kale na Agano Jipya zilivyo na uhusiano.

MAZOEZI:

Ni wakati wako wa kujaribu! Hebu tuangalie katika Mwanzo 1:3- “Hebu kuwe nuru” na ikawa nuru”

34

1. Tafuta herufi ya mstari rejea kwenye kifungu.
2. Nenda kwenye mstari unaofanana kwenye kolamu ya rejea.
3. Tafuta herufi kwenye kolamu ya mistari rejea ambayo inafanana na herufi iliyoapatikana kwenye kifungu (“mwanga”)
4. Iwekee Alama mistari miwili ya rejea iliyoorodheshwa.
5. Angalia mstari wa kwanza kati ya mistari miwili ya rejea.(2Wakorintho 4:6).
6. Uliza swali: Mstari huu unagusaje maisha yangu kiasi cha kuleta mabadiliko katika ufahamu wangu?
7. Andika ulilopata moyoni mwako juu ya somo hili na swali la nyongeza.
8. Nenda kwenye mstari mwingine wa rejea, uliokuwa umeorodheshwa kwenye mstari wa rejea wa Mwanzo1:3 (1 Yohana 1:5-7).
9. Tena, uliza swali: Ni fundisho gani ninalopata toka mstari huu la kunipanua uelewa wangu?
10. Andika fundishao lolote, na nyongeza ya swali.

SOMO LA TATU — SEHEMU YA 3

ZANA #4:

Itifaki: Ni orodha ya kimsingi katik kitabu, iliyopangwa ki-alfabeti.

Itifaki imewekwa nyuma mara nyingi ikifuatwa nikifuatana na ramani. Kila kampuni ya uchapaji hutengeneza orodha yake tofauti ya maneno kwaajili ya itifaki ya Biblia yake. Baadhi ya itifaki ina majina na vitenzi, wakati nyingine huogeza Miji ya ki Biblia na maeneo yake, na nyingine huorodhesha mianzo ya maneno muhimu, ikijumulisha majina ya watu wa Biblia.

MAFUNDISHO - (matumizi ya itifaki ya Biblia):

1. Itifaki itasaidia kuonyesha mstari husika wenyekuwa na **нено**. Kwamfano, ukitaka kutafuta mstari na unakumbuka kuwa ni neno “mchungaji”, kwa wepesi kabisa angalia neno mchungaji kwenye itifaki itakusaidia kupata mstari.

Kwa mfano, unaweza kuwa unafahamu mstari “Bwana ndiye mchungaji wangu” lakini hujui unakopatikana. Kwa kuangalia neno “mchungaji” katika itifaki, utakuta kuwa neno hilo linapatikana katika Zababuri 23:1.

MAZOEZI:

Sasa unajaribu! Neno ni “hazina” na unakumbuka maneno “hazina yako ilipo, ndiko itakakokuwa roho yako.” Kwakutumia itifaki tafuta kifungu ilikowekwa. Ulifanya nini? Angalia jibu lako. Liko katika Mathayo 6:21

2. Itifaki itasaidia kuonyesha **tukio** fulani katika Biblia. Unajua kuwa Eliya alikwenda mbinguni kwenye gari ya moto, lakini hujui habari hiyo iko sehemu gani ya Biblia. Ukingalia neno “Eliye” utaweza kupata simulizi katika 2Wafalme 2:11-12

MAZOEZI:

Zamu yako! Neno ni “Sulemani” na unajaribu kutafuta simulizi wakati alipo amua kesi kati ya makahaba wawili. Habari hii inapatikana wapi? Soma habari hii mwenyewe!

Tena, angalia majibu yako. Inapatikana katika 1Wafalme 3:16-28.

SOMO LA TATU — SEHEMU YA 4

MAFUNDISHO (Matumizi ya Itifaki ya Biblia):

3. Itifaki itakusaidia kuonyesha *rejea nyingine* ambako neno Fulani linatumika. Utajua kuwa neno “mchungaji” linapatikana katika Zaburi ya 23:1. Ni rejea gani nyingine zinazohusiana na neno mchungaji? Itifaki inaorodhesha vifungu vingine ambako “mchungaji” linatumika kama vile Isaya 40:11 na Yohana 10:11.

MAZOEZI:

Neno ni “miguu” na ungetaka kutafuta mistari rejea mingine kwaajiri ya “miguu”. Itifaki huorodhesha miguu (mguu). Zaburi 8:6, Zaburi 119:105; Warumi 10:15 na 1

Wakorintho 12:21, zote zimeandikwa kama rejea. Kazi yetu imeanza. Kwanza, Angalia rejea kwa kila neno moja, na kisha kwenye daftari yako ili uone kila mistari unasemaje na uanze kuweka alama kile unachojifunza kwenye maandiko kuhusiana na neno “miguu.”

4. Itifaki itasaidia kujufunza *Neno*. Kwa mfano, kutumia neno “nuru,” nenda kwenye itifaki kwaajiri ya msaada tafuta kupitia maandiko ambayo yanaelekeza “nuru”. Orodha ni ndefu lakini utagundua kuwa orodha inaanza Mwanzo 1:3 na inaendelea kutaja katika vitabu mbalimbali hadi Ufunuo 21:23.

MAZOEZI:

Neno “dhabihu” na unajifunza juu ya neno ni vitabu vingapi vilivyoorodheshwa vinavyozungumzia dhabihu?

5. Itifaki itakusaidia kuelewa **maana** ya neno hilo. Kumbuka neno mfuasi. Tunafahamu kuwa Yesu alikuwa na wafuasi. Mfuasi ni nani? Kama ningekutaka uoelezee maana ya neno, itifaki ingekupa msaada katika hiyo kazi yako uliyopewa kwa kuorodhesha mistari ya rejea kwaajili kuangalia.

ZOEZI:

Mwanafunzi ni nini? Ni ipi mistari ya rejea na kila mmoja unatoa uelewa gani kwa maana ya neno? Tumia daftari yako kuandika utafiti wako.

Maoni: Tumia Mathayo 28:19, Yohana 8:31, Yohana 13:35, na Luka 14:27.

Kwa ufupi, ulijifunza kutoka Mathayo 28 kwamba Mungu anataka kila mmoja awe mwanafunzi pasipokujali mila na mazingira ya mtu alikotoka (mataifa yote). Ulijifunza katika Yohana 8 kwamba mwanafunzi huamini na kufuata mafundisho ya Mwalimu wake, na kutoka Yohana 13 kwamba wanafunzi hupendana, kutokana na mahusiano yao na mwalimu wao ambaye huwapenda. Nao pia hujiunga katika uhusiano huo wa kupendana na kuwapenda wengine. Na katika Luka 14 kila mmoja hufahamu kuwa ufuasi tu haitoshi bali kuna gharama ya ufuasi.

MATUMIZI:

Unafanyika mwanafunzi kadiri unavyosoma Neno Lake. Unajionaje kuwa mwanafunzi kufuatana na mistari hii?

SALA:

Ninataka kuwa mwanafunzi. Nataka nikufuate, Yesu. Nataka kujifunza kutoka kwako na kadiri ninavyoendelea kujifunza kukua kwa kina katika uhusiano wa upendo na wewe. Amen.

SOMO LA TATU — SEHEMU 5

MAFUNDISHO - (Nyongeza katika matumizi ya itifaki):

6. Itifaki itakuunganisha na **mstari wa rejea** . Mara tu unapotafuta mstari mmoja wa rejea unakuunganisha na mistari mingine ya rejea. Kumbuka neno “Bethlehemu”. Kwanza, litafute katika itifaki. Mstari mmoja wa rejea umetolewa. Kwa mfano, nikianza na mmoja ulioorodheshwa kwenye Biblia yangu ambao ni Mathayo 2:1, Nitakuta mstari wa rejea hapo. Ingawa itifaki inanipa rejea moja, kwa kufanyia kazi mstari wa rejea utanipa nafasi ya kupata maeneo mengine kwenye maandiko ambayo yanaonyesha Bethlehemu.

ZOEZI:

Neno ni “tahiriwa”. Tafuta rejea kwenye Biblia yangu inatoa moja. Mara tu ukipata ya kwanza, inawezekana .Angalia kama rejea yenye maneno ya italiki yapo, ili kukuelekeza kwenye mtandao wa vifungu vingine. Tumia muda kufuatilia kwenye kumbukumbu zako ulizoandika juu ya uliyojifunza kuhusu tohara.

MARUDIO:

▪ Umeishajifunza *zana* nne jinsi ya kupitia kitabu kwa haraka zaidi. Jipatie muda kuziorodhesha. Usisite kutumia kumbukumbu zako ulizoandika kwenye daftari yako!

1.

2.

3.

4.

▪ Utafafanua je maneno haya?

1

Agano

Kale _____

—
2 Agano

Jipya: _____

—
40

3. Sura: _____

4. Mstari: _____

5.

Kifungu

au

rejea: _____

6.

Vitabu

vya

Musa: _____

—
7.

Injili: _____

Mfano: _____

9.

Waraka: _____

Jaza nafasi nne hapo chini ukionyesha mambo manne ya muhimu ambayo ni faida kwako, katika kujifunza hadi sasa:

• _____

• _____

• _____



SOMO LA NNE — SEHEMU YA 1

UTANGULIZI:

Mtu anachukuaje kifungu cha Biblia na kujifunza kutoka humo? Ni kwa jinsi gani maneno yanakuwa ya maana na kuchukua nafasi katika hali halisi ya maisha yangu? Katika somo hili tutaona zana nyingine katika kukabili kifungu cha Biblia na kupata ukweli kwaajili ya kukihusianisha na kukitumia katika maisha binafsi.

FUNDISHO:

Maswali ni njia tunayotumia katika kufahamiana na watu wengine katika maisha yetu. Ni njia pia tunayotumia katika kujenga mahusiano na watu walio wageni kwetu. Kwa kutumia maswali wanafahamika zaidi kwetu. Tunapowauliza maswali tunakuwa na matumaini kuwa tutapata ufahamu zaidi juu yao.

Hii ni sawa na Mungu. Mungu hutuwezesha kumfahamu kupitia kusoma Neno lake. Anataribisha tuulize maswali, na hatimaye tunajifunza Biblia. Anajifunua kwetu, Anatwambia Yeye ni nani, na Anatwambia ni kiwango gani Anatupenda. Tunauliza maswali na kadiri tunavyojifunza Biblia tunafahamiana naye na tunajifunza kuwa Anahitaji kuwa na uhusiano unaoeleweka, pamoja nasisi. Zaidi ya hayo, anapenda kutusaidia na kutupa mwongozo jinsi itupasvyo kuishi, jinsi ya kufanya uchaguzi na maamuzi yenye manufaa kwetu na watu wengine. Tuna nafasi katika maisha yetu yaliyobaki kufahamiana naye zaidi. Andika maswali yako upandeni mwa daftari yako. Furahia kufahamiana naye!

ZANA #5:

Maswali! Uliza maswali! Anza kwa kudhamiria kama sehemu ya Biblia unayojifunza ni *mazingira* au *tukio* hata kama ni tukio *fundisho*, kamavile mfano au andiko kutoka moja ya Nyaraka. Maswali na mazoezi ya leo, yatalenga zaidi kwenye maswali yahusianayo ya hali mazingira au hali halisi au tukio. Sehemu inayofuata italenga kwenye maswali yahusianayo na mafundisho. Maswali haya yatakusaidia kuanza kadiri unavyoanza kuwa na maswali ya yenye kufurahisha na kuanza kugundua majibu!

Ikiwa sehemu unayojifunza ni *mazingira au tukio*,

1. Ni nani anaye elezea habari na kwanini anailezea?
2. Nani wahusika?
3. Mfumo wa habari ukoje?
4. Kwa mtazamo wa kwanza, ujumbe ni nini?
5. Ni kwa sifa gani nitagundua?

Kuifanya Biblia Iwe Yako

42

6. Ni jambo gani lililo la “kufikirika” (mystery) lililo kwenye habari?
7. Habari inaniambia nini kuhusu MUNGU? Kuhusu mwanadamu?
8. Ni mambo gani nisiyofahamu kuhusu habari hii?
9. Ni nini mwitikio wa wahusika katika habari hii?
10. Ni nini ninacho amini kuwa Mungu anasema na mimi binafsi?

ZOEZI:

Ni wakati wa kujaribu wewe mwenyewe:

- Fungua kwenye simulizi inayopatikana kwenye Luka 13:10-17. Tumia maswali yaliyoorodheshwa *hali halisi* na *matukio* na anza kufanyia kazi kifungu. Andika maswali kwenye daftari yako na yafuatilie katika mwitikio wako.

Ikiwa hujui jibu la swali, kubali na uendelea na linalofuata.

MATUMIZI:

Baada ya kufanyia kazi habari iliyo kwenye Luka 13:10-17, andika maswali mawili uliyojiuliza ambayo yanajaribu kujibu maswali: Ni kwa vipi habari hii inaweza kutumika kwangu na katika maisha yangu?

Mfano wa maswali: Ni kwa vipi ninafana na mwanamke huyu aliyepindana?

• Swali

#1: _____

• Swali

#2: _____

SALA:

Wakati mwingine, Bwana, Ninajihisi kupindana kwa mizigo ya dhambi na nafsi inayonishitaki katika maisha yangu. Siwezi kusimama wima. Ninasikia ukiniambia, “ _____, Umewekwa huru” na ninakuwa huru kutoka mabo yangu ya kale. Sasa ninaweza kuishi maisha ya kusimama wima, asante, Msikilizaji wangu . Amen.

SOMO LA NNE — SEHEMU 2

FUNDISHO:

Zana #5 ilianzishwa kwenye somo lililopita: Swali! Swali ambalo tulifanyia kazi lilielekea kwenye maswali ya kuuliza wakati wa kusoma mazingira au matukio. Somo la leo litalenga katika kuuliza maswali wakati wa mafundisho ya Yesu au maneno yaliyoandikwa na waadishi wa nyaraka za Agano Jipya. Kwa mfano, Kumbuka, kabla hujauliza maswali unahitaji kuamua kama sehemu unayojifunza inahusu mazingira, tukio au ni fundosho.

Ikiwa sehemu unayojifunza ni *fundisho* ...

1. Nani alisema maneno haya?

2. Ni neno gani la msingi, neno, au kifungu katika mafundisho haya?
3. Kifungu hiki kinge sikikaje katika lugha yangu?
4. Ni maneno gani ya picha ninayoweza kutumika ili yanisaidie kuelewa?
5. Ninajifunza nini kuhusu uhusiano wangu na Mungu?
6. Ni eneo gani katika maisha yangu mistari hii inanipa changamoto?
7. Kifungu hiki kinafunua nini kuhusu sura ya Mungu?
8. Ni maswali gani ninataka?
9. Ni ukweli gani ambao naamini kuwa Mungu anitaka nifahamu?
10. Itikio langu ni nini kuhusu ukweli huo?

ZOEZI:

Ni wakati mwingine sasa ujaribu:

Fungua kwenye mafundisho ya Mathayo 7:24-29.

Kwa wakati huu tumia maswali ambayo yameorodheshwa hapo juu kwaajili ya mafundisho. Kama ilivyokuwa sehemu iliyopita...anza kufanyi kazi inayofuata! Andika maswali kwenye daftari yako na yafuate kwa itikio. Kama hufahamu majibu ya maswali, kwa urahisi kubali na endelea na yanayofuata!

MATUMIZI:

Baada ya kumaliza kufanyia kazi mafundisho toka Matthayo 7:24-29 andika maswali mawili uliyojifuliza ambayo yanajaribu kujibu: Ni yapi matumizi ya mafundisho katika maisha yangu? Mfano: Je, nimechagua kujenga nyumba ya maisha yangu kwenye mchanga au kwenye mwamba?

Kuifanya Biblia Iwe Yako

• Swali

#1: _____

• Swali

#2: _____

SALA:

Bwana Yeau, Ninataka maisha yangu yanjengwe. Ni wewe unipaye nguvu kwenye maisha hayo.

Ni Wewe unayeniwezesha kuvumilia hata kama upepo na mvua hunipiga na hutafuta kuniangamiza. Asante kwa kuwa mwamba wangu. Amen.

SOMO LA NNE — SEHEMU YA 3

ZANA #6:

Jifunze kutambua **maneno makuu ya sentesi** katika kifungu unachojifunza. Angalia maneno yanayorudiwa, maneno ambayo ambayo msemaji au mwandishi anapenda kuyasisitiza.

MAZOEZI:

Hapa kuna mifano michache maneno makuu yenye umuhimu zaidi kwa kurudiwa kwake na msisitizo wake. Angalia unachopata baada ya kujifunza!

Rejea

Neno la msingi

Umuhimu

2 Wakorintho 1:3-7

1 Yohana 4:7-12

Yohana 4:13-14

Ulifanyaje? Kutokana na rejea hizi tatu jifunze kuwa, kutia moyo, upendo, na maji ni maneno ya msingi kwenye mistari hii. Kila neno la msingi linatumika kuisisitiza fundisho. Fundisho la kwanza limeandikwa na Mt. Paulo. Anawataka Wakristo katika Koritho kufahamu kuwa faraja ya kweli hutoka kwa Mungu. Yohana katika Walaka au barua

zake anataka wasomaji kufahamu kuwa upendono tulionao unatokana na upendo ambao Mungu alikuwa nao kwaajili yetu. Na katika Injili ya Yohana, Yesu anamwambia mwanamke kwamba Yeye ni maji ya uzima na akiishi ndani yetu Anatupatia maji ya uzima wa mile!

ZANA #7:

Kujifunza **mpangilio** ambamo simulizi au matukio yanatokea, inaweza kuongeza ufahamu juu ya kifungu husika. Kwa mfano mazungumzo kati Yesu na Nikodemo yanafanyika usiku.

Je ingeleta tofauti gani iwapo Nikodemo angekuja alasiri kwa Yeu badala ya kuja *usiku* sawa na ilivyo katika Yohana 3:1-2 . Kitendo chake cha kuja usiku, kinaibua maswali machache.

Kwa mfano: Je tunaweza kudhani kuwa hakutaka Yesu amuone? Kama hakutaka kuonwa naye, ni kwa nini? Kwanini Nikodemo alichukua hatua ya gharama kuja kumuona? Ni jambo gani lililo msukumo Nikodemo alikubali kuchukukua hatua hiyo ya gharama?

ZOEZI:

Hizi rejea tatu zinataja miundo mitatu tofauti ambamo alikutana na watu. Ni miundo gani na ni maswali gani ambayo yanaleta mawazo mapya au hisia za ndani, kwaajiri ya kuelewa mazingira?

Rejea

Mifano

Maswali

Mathayo 4:1

Marko 1:35-37

Yohana 20:19-20

Yesu alikutwa jangwani, katika mahali palipojitenga, na kwenye chumba kilichofungwa ambamo wanafunzi wake walikuwa wamejificha. Kwanini Yesu alikuwa sehemu mojawapo ya hizi? Mathayo anatwambia kwamba Yesu alikuwa jangwani ili ajaribiwe. Marko anatwambia kuwa Alikwenda maahali palipojitenga kuomba. Na Yohana husema kwamba alisimama kati ya wanafunzi kwenye chumba, na jambo la kwanza

alilowaambia lilikuwa ni “Amani”. Uliisha jikuta jangani, mahali pa majaribu?

Yesu anakutana nawe hapo. Ni vipi kuhusu mahali pa upweke na ulimkuta Yesu huko? Je uliisha jikuta kwenye mazingira ambamo ulijihisi kuwa “umefungwa” lakini ulifahamu kuwa Yesu ameingia kwenye hali yako hiyo na amechagua kusimama nawe akileta neno la amani na matumaini? Tuna mazingira tofauti ambamo Mungu anatukuta.

SALA:

Yesu, Unakuja kwangu katika hali tofauti ya ya mifumo na mazingira. Unakuja kwangu kufanya uwepo wako kuwa halisi kwangu katika maisha yangu ya kila siku. Asante kwa kusimama pamoja name kuniwezesha kuvumilia majaribu na hofu. Wewe ni amani yangu. Amen.

SOMO LA NNE — SEHEMU 4

MARUDIO:

Tukianza na somo 1, umeandaliwa kwa zana saba tofauti zitakazo kuasaidia kusafiri kwa ukamilifu kupitia Biblia. Baadhi ya zana ni nyepesi kutumia kuliko nyingine. Baadhi ya zana huitaji mazoezi zaidi, lakini zote ziko kwenye sanduku lako la zana na ziko karibu na wewe. Unavyo endelea kusoma Biblia, zana hizi zitazidi kukusaidia ili ufahamu ni nini Mungu anasema. Anataka ufahamu upendo wake mkuu kwaajiri yako.

ZOEZI:

Kwa hiyo, hebu turudie! Andika zana saba! Anza na Somo 1.

1.

__ (Somo 1)

2.

__ (Somo 2)

3.

__ (Somo 3)

4.

__ (Somo 3)

5.

__ (Somo 4)

6.

__ (Somo 4)

7.

__ (Somo 4)

FUNDISHO:

Ni muhimu kufahamu kuwa kuelewa kuwa, kujifunza Biblia ni kanuni. Kanuni katika hali hii siyo adhabu. Tunapoelekeza katika kusoma Neno la Mungu, inamaanisha zaidi kuelekeza, au kuandaa. Wanariadha wana kanuni nyingi za kufuata wakiwa wanajiandaa kwaajiri ya tukio Fulani. Kadiri kanuni zinavyokuwa nyingi, ndivyo ulivyo uwezekano wa kukamilisha malengo waliyo kusudia ya kushinda na kuchukua zawadi na kuzipeleka kwao.

Kanuni ni kwa makusudi ili mtu aweze kutenda kama alivyochagua, na kuwa katika hali ya mafunzo. Kujiwekea kanuni na nidhamu inatupa changamoto ya kufanya kazi ndani ya mfumo na utaratibu, na mipaka fulani. Mwingine hujiweka chini ya utaratibu au kanuni ili asababisha matokea mema na makubwa zaidi. Mungu anatumia taratibu, kanuni na nidhamu ili kufanya marekebisha ndani mwetu, ili atengeneze ndani yetu tabia ya ki-mungu.

Katika somo hili utapewa changamoto kwaajiri ya utaratibu au kanuni nyingine. Kanuni ni kukariri. Kukariri mistari, hata sura, za Biblia inaweka Neno la Mungu katika mioyo yetu, na inatupatia chakula kadiri tuendeleavyo kuishi maisha yetu ya kila siku. Tunahitaji Neno lake liwe kwenye mawazo yetu.

Ili liweze kuwa kwenye mawazo yetu ni lazima tujifunze juu yake. Tunahitaji ufahamu kuhusu maneno, maana yake ni nini, na Biblia inalosema. Kupitia Biblia yote tunajifunza Neno la Mungu. Sasa, tuna changamoto ya kuchukua hatua ya mbele zaidi zaidi juu ya mafunzo haya. kwa mfano Mwanariadha, husoma kitabu cha maelekezo, huvaa vifaa na huwa na upendo wa ndani juu ya mchezo, mwanariadha pia hujua makusudi ya mchezo; anakuwa amepanga utaratibu atakaofuata katika kucheza, na anakuwa ameelewa vizuri mipango yake ili acheze kwa kujiamini, na ufundi wa hali ya juu.

ZOEZI:

Zingatia mistari ifuatayo, na tafakari isemavyo kuhusu kuweka Neno la Bwana mioyoni mwetu.

Rejea

Itamke tena mistari kwa kutumia maneno yako.

Zaburi 1:1-2

Kumbukumbu 6:6-9

Zaburi 119:11

Mithali 6:23

Wafilipi 4:8,9

Wakolosai 3:1-2

Waebrania 4:12

FUNDISHO:

Kutokana na mistari hii tunajifunza:

- Mungu anataka Neno lake liwe mioyoni mwetu na kwenye mawazo yetu. Tunaalikwa kutafakari Neno lake usiku na mchana .

Somo la 4 Sehemu 4

- Tunajifunza kuwa Neno lake ni zana ya kufundishia watoto wetu ili wamfahamu na kumtii Yeye, na Neno lake.

- Zaburi 119 inatukumbusha kwamba Neno lake likiwa limefichwa mioyoni mwetu, tunahepuka kumkwaza Mungu kwa kumtenda dhambi.

- Katika Methali tunahakikishiwa kuwa mafundisho yake, amri zake, na maonyo yake ni njia ya uzima.

- Katika Wafilipi tunatiwa moyo kufikiri mambo yaliyo mema na mazuri ili amani ya Mungu iingie maishani mwetu.

- Paulo anatumkumbusha kuelekeza mioyo yetu na mawazo yetu kwa mambo yaliyo juu.

- Mwandishi wa kitabu cha Waebrania antuhasa tufahamu kuwa Neno lake linafanya kazi ndani yetu, litabadilisha fikra zetu na tabia ya mioyo yetu. Biblia inatuhimiza kutunza Neno la Mungu ndani ya mioyo yetu na kwenye midomo yetu. Kwa kupitia mafunzo haya ya Biblia, tunashauriwa kukariri mistari ya Biblia. Mstari mmoja au miwili kwa juma huongeza hekima ambayo moyo wako utashika na kupatikana kwako wakati utakapouhitaji kwa matumizi. Ni changamoto ya kufurahisha kiasi gani! Uko tayari?! Hebu tuanze kujenga kumbukumbu za maktabu zetu!

FUNDISHO:

Ushauri kuhusu kukariri:

- Onyesha kifungu.

- Kiandike kwenye vipande vya karatasi ili uvipate kwa wepesi.
- Furahia changamoto za kukariri!
- Pata nafasi ya kushirikishana na mtu mwingine, anaweza akawa ni mtoto au rafiki.
- Baadhi ya mistari ina taswira kubwa. Mfano, kumbuka taa kutoka Zaburi 119:105 kama mwogozo na nuru, kama njia ya kutawanya giza.
- Andika “mabo ya kukumbuka” kwenye karatasi au kadi, kadiri yanavyokuja kwenye mawazo yako, kadiri unavyo endelea kutafakari Neno. Hii inaweza kujumlisha maswali au mawazo au njia ni kwa vipi maneno haya yanaweza kutumika kwenye maisha yangu ya leo.

Hapa kuna mfano...

Zaburi 142:7

“Niweke huru kutoka kwenye kifungo change, ili nilitukuze jina lako.”

Mawazo muhimu: Bwana ananitaka niishi maisha huru pasipo kurudishwa nyuma na lolote.

Ananitaka niwe huru nimsifu.

“Kumsifu” kuna maana gani? Unafanyaje hivyo?

SALA: Bwana, Neweke huru kutokana na lolote ambalo linawenza kunisababisha nisikusifu.

Nifundishe jinsi ya kukusifu!

ZOEZI:

- Kariri Zaburi 119:105. Fuata “maelekeza kwaajili ya kukariri” kama yalivyoorodheshwa hapo juu.
- Changamoto nyingine ya kufurahisha kuhusu kukariri inapaswa iwe kukariri mfuatano wa vitabu 66 vya Biblia. Iweke kwenye mawazo yako kuwa ukikariri vitabu 11 kwa siku kwa siku 6 changamoto itakuwa imemalizika! Mbinu iliyotofauti ingekuwa kukariri vitabu 6 kwa siku na changamoto ingekuwa imekamilishwa kwa siku 11!! Itumie! Unawe kuifanya!

- Hapa kuna mapendekezo: Kariri vitabu vya Biblia kwa mfuatano ukitumia 66, 3 × 5 kadi. Andika majina ya vitabu katiak upande mmoja. Andika namba upande mwingine wa kadi kwa mfuatano. Changanya na upange upya kadi kwa mfuatano!

SOMO LA NNE — SEHEMU YA 5

FUNDISHO:

Tumezungumzia kuhusu *masomo* na *kukariri* Neno la Mungu kuwa kanuni mbili zenye maana.

Somo hili litaelezea kanuni ya tatu, ambayo ni ya *maombi*. Katika somo la tano tutajifunza zaidi kuhusu maombi na kukua kwa kina kwa ufahamu wetu na kuwa na shukrani kwa kipawe cha Mungu tulichopewa. Kadiri tunavyokua katika ufahamu wetu juu ya maombi tutapalilia uhusiano wetu naye. Mungu anatumia neno lililoandikwa, Biblia, kama njia ya kuwasiliana. Maombi ni mwaliko wa Mungu kwetu kuzungumza naye.

➤ MAANA:

Maombi ni kitendo cha ibada ambamo tunawasiliana na Mungu.

KUMBUKA: Vitabu na maandishi ya aina zote yameandikwa kuhusu maombi. Mada haiwezi kufundishwa na kumalizika. Kwa lengo la somo letu hili hebu tuifanye nyepesi.

Hapa kuna maneno machache ya utangulizi:

1. Mungu anatumia ili tuombe. Mwaliko wa kuja kwenye uwepo wa Mungu Mwenye enzi umetolewa na Mungu mwenyewe.

. Andika Zaburi 50:15.

2. Ahadi ya Mungu ya kusikiliza maombi yetu. Andika 1 Yohana 5:14 -

Husikiliza maombi yetu na anaahidi kuyajibu. Andika 1 Yohana 5:15 -

3. Mungu anakuja nyuma ya mlango uliofungwa, kuwa pamoja na sisi, na kupokea maombi yetu

Andika Mathayo 6:6

SALA:

Asante kwa kunikaribisha nizungumze na Wewe. Asante kwa kuniahidi kusikiliza mawazo na matahitaji ya moyo wangu. Asante kwa kuahidi kusikili kilio change wakati ninapojihisi kutokuwa na msaada, na kuwa mpweke.

Ninashukuru kwa kuwa Unajua na kufahamu mambo yaliyofichika niliyonayo moyoni mwangu. Asante kwa kunipenda pasipo kujali yale unayofahamu juu yangu. Amen.

SOMO LA TANO—SEHEMU YA 1

FUNDISHO: -

MAOMBI – Hebu tuchimbe kwa ndani!:

Uwiano kati ya kusikiliza na kuongea ni muhimu kwa mahusiano yoyote yenye afya. Wakati mwingine tunaongea na wakati mwingine tunasikiliza. Sawa na ufundi unavyoendelezwa na kufanyiwa kazi, mahusiano pia huendelezwa katika usalama wenye kina, kukubalika, kuelewa, na kutafakari kwa kina.

Tunapoongea tunaongeza ufahamu juu ya nafsi zetu na watu wengine ambazo huweza kutufanya tuseme ‘aha!’ baada ya mda. “Nimelipata!” “Nimeelewa!” “Nilikuwa sijafikiria hivyo kabla!” Haya ni maelezo ya kawaida ya ‘aha!’ katika maisha yetu. ‘Aha!’ hutokea katika maombi. Tunapoanza kutamka mambo mioyoni mwetu, Mungu kupitia kweli Amejiweka katika Neno lake na kwa kutenda kazi kwa Roho Wake, anatupatia ufahamu wa ndani, kutambua, hekima, ufahamu, na nidhamu kwa kusudi la kuishi maisha ya milele kama watoto Wake. Maombi ni sehemu muhimu ya maisha ya mtu kutafakari. Mungu husema kupitia Neno Lake na tunasikiliza.

Hatimaye, wakati hufika ambapo sisi huongea, na Mungu husikiliza, Maombi ni kazi ngumu. Ni rahisi kwa mtoto kulalamika au kutumia maneno mengine kuwasiliana na mzazi.

Pamoja na hayo, muda wa kukumbukwa, kwa mahusiano kati ya mzazi na mototo, ni pale mtoto anapobeba moyo wake akamwambia mzazi kwa unyenyekevu, mizigo aliyo nayo. Mizigo imebebwa na mzazi sasa mtoto ni huru. Muda mwingine wa kukumbukwa kwa mahusiano ya wazazi na mtoto, inawezekana ikawa wakati mtoto anapomhusisha

mzazi kwenye tukio fulani la furaha; kama vile mafanikio katika michezo, sherehe ya kuzaliwa kwa mtoto, kufahuru masomo magumu, au kuhitimu masomo ya chuo. Tunaweza kuorodhesha mambo mengi yahusuyo tafrija au kusherekea kwa namna fulani.

Kama maombi ni jambo jipya kwako, zana ya msaada ya kujifunza jinsi ya kuomba ni kukariri maneno haya manne, na uyatumie kila siku ili yakusaidie kukua katika mahusiano yako na Mungu katika maombi:

1. Maombezi.

➤ *Maana: **Maombezi*** ni kitendo cha kufurahia Mungu jinsi Alivyo na kuabudu au kumtukuza kwa matendo na tabia yake.

Kumbuka: Baadhi ya maneno ya kutukuza ni: sifa, heshima, utukufu, kuinua.

2. Kukiri

➤ ***KUKIRI:Kukiri*** ni kutambua hali ya ubinadamu wetu mbele za Mungu pasipo kujaribu kutunza siri au kuficha Mungu au nafsi zetu uhalisia wa dhambi zetu tulizomtenda yeye na binadamu wenzetu.

Kumbuka : Baadhi ya maneno ya ukiri ni: tubu, kiri, tambua.

3. Shukrani

➤ *MAANA: **Shukrani*** ni maelezo ya shukrani kwa Mungu yanayotolewa kama ibada yetu, ambamo tunakiri na kutambua wingi wa upendeleo wake katika maisha yetu.

Kumbuka: Baadhi ya maneno ya shukrani ni: kutoa shukrani, asamte, kushukuru.

➤ *MAANA: **Ibada*** neno hili lina mzizi katika neno “ustahili” na ni tendo la kutoa heshima kwa Mungu ambaye peke yake anastahili kuheshimiwa kama Mungu.

4. Maombezi

➤ **MAANA:** *Maombezi* ni tendo la maombi la kuja mbele za Mungu na kumpa mahitaji ya mioyo yetu. Wengi wanaohusika wanaelezewa kufuatana na mahitaji ya binafsi au mazingira fulani au kumshirikisha mahitaji ya mtu mwingine.

Kumbuka: Baadhi ya maneno ya maombezi ni: kuomba, kuomba, kusihi.

Ni maisha ya maombi ambamo tunaelezea mahitaji yetu lakini pia tunawakumbuka wengine na mazingira yao.

Mungu anatupatia Neno lake kutusaidia kuomba. Tunaweza Neno lake kufahamu ni kwaajili ya nini inatupasa kuomba. Ukiendelea kukumbuka Kutukuza au kusifu juma hili, kwa mfano, rejea za Biblia zitakusaidia kukuongoza. Rejea hizi ni msaada tu ili uanze ziara yako ya maombi. Tumia daftari yako kuorodhesha maombi ya nyongeza na mawazo ambayo yatakuja kwenye fikra zako. Usisite kurudi nyuma na kujikumbusha juu ya maana ya maneno na kuelewa zaidi maana ya maneno hayo.

SOMO LA TANO — SEHEMU YA 2

FUNDISHO:

Ombi1. SIFA: Kwa urahisi sifu, na tukuza, na ushukuru Bwana kwa kuwa ya Alivyo. Kadiri unavyoendelea na masomo yako utaongeza ufahamu wako juu ya Mungu ni nani. Fikiria kwa mda mfupi juu ya kile ulichojifunza kuhusu Mungu kati ya mojawapo ya rejea tulizojifunza.

ZOEZI:

Bwana , Ninakutukuza na kukushukuru kwasababu ya ulivyo. Asante kwa kuwa Mungu wa mianga ambaye hutawanya giza na unaleta ufahamu juu ya maisha yangu.

Kamilisha sentensi hizi:

• Nakushukuru kwakuwa wewe ni _____
Tazama 1 Yohana 4:16.

• Nakushukuru kwakuwa wewe ni _____
Tazama Mwanzo 17:1.

• Nakushukuru kwakuwa wewe ni _____
Tazama Yohana 21:17

Nyongeza ya mawazo ya maombi...

- _____

- _____

- _____

SOMO LA TANO — SEHEMU YA 3

FUNDISHO: Maombi

2.UKIRI:

Mung anafahamu mambo haya katika maisha yetu ambayo hututenga naye. Anakukaribisha kumruhusu akuweke huru kutokana na mashitaka yako yote nafsini mwako, na kukupa maisha yaliyo wazi mbele Yake.

ZOEZI:

Bwana , Ninajifahamu vizuri. Nafahamu kuwa mimi ni mwenye dhambi. Nakiri kwako kwamba sijawatende wengine kwa upendo.

Kamilisha sentensi hizi:

• Bwana, Nakiri kwako

_____ Tazana Warumi 12:3.

• Bwana, Nakiri kwako

_____ Tazama Warumi 12:16.

• Bwana, Nakiri kwako

Tazama, Warumi 12:17.

Mawazo ya nyongeza ya maombi...

- _____

- _____

- _____

SOMO LA TANO — SEHEMU YA 4

FUNDISHO: Maombi

SHUKRANI:

Na tena, tuna mengi tuliyoandika kuhusu shukrani. “Asante” ni jambo ambalo sote tuna ngojea kusikia. Kusema asante unasonyesha kuwa unathamini fulani alivyo au kwa yale aliyoyafanya. Asante ni kumwambia mtu mwingine kwamba amegusa maisha yako katika hali ya manufaa. Tunaweza kukumbuka kwa haraka wakati mtu alipotushukuru kwa jambo ambalo hata hatukumbuki tulilofanya. Tunaweza kukumbuka wakati asante kutoka kwa mtu ilithibitisha tabia yetu ya kweli. Kwa jinsi hiyo hiyo, ni vizuri kumshukuru Mungu kwa jinsi alivyo na kwa yale aliyoyafanya. Ni vema kumshukuru kwa jinsi anavyogusa maisha yetu kupitia watu na mazingira mbalimali. Naye pia anasubiri kusikia maneno yetu ya shukrani. Sawa na tunavyomfundisha mtoto kusema “asante” sawa na ilivyo vema mtoto kukumbuka tuliyo mfundisha, hivyo hivyo na sisi tunapaswa kukumbuka. Tunaposema asante tunakumbuka yote ambayo ametufanyia. Kumbuka kusema asante. Ni jepesi sana.

ZOEZI:

Bwana, Nakuja mbele zako na moyo wa shukrani. Kamilisha sentesi hizi:

• Bwana, _____ Nakushukuru _____ kwa
kwa _____

Tazama 1 Wathesalonike 5:18.

• Bwana, _____ nakushukuru _____ kwa

Tazama Zaburi 103:3.

• Bwana, _____ Bwana _____ nakushukuru _____ kwa

Tazama Waefeso 2:8-9.

Maombi ya nyongeza...

- _____
- _____
- _____

SOMO LA TANO — SEHEMU 5

FUNDISHO:Maombi

4. MAOMBEZI: Maombi si kwamba tunamwambia jambo ambalo Hafahamu, Japokuwa tunakwenda kumwambia jambo jipya. Anafahamu mambo yote (Yohana 21:17). Kwa hali halisi maombi ni kwa faida yetu. Maombi ni mwaliko wa Mungu kwetu kuja kwake kwa hiari kumwambia kila kitu ndani ya mioyo yetu (Zaburi 55:22). Uzoefu ni sawa na picha ya mtoto ambaye huamini kuwa wazazi watampatia mahali salama ambamo ataongea kwa uhuru na ukweli, ana hamu ya kusikiliza, na anaweza kusuruisha sehemu kubwa ya mazingira magumu.

5 ZOEZI:

Kamilisha sentesi za maombi:

• Bwana, Nahitaji

• Bwana, nahitaji

• Bwana, nahitaji

Maombi ya nyongeza...

• _____

• _____

• _____

Bwana usikusudie maombi kuwa ya kuongopesha au tishio. Kinyume na hayo maombi ni fursa. Ni wakati Mungu anapotualika kuja mbele zake jinsi tulivyo. Ana hamu ya kusikia chochote kile tunachotaka kumshirikisha. Anaheshimika kwa kuja kwetu kuzungumza naye.(Zanuri 50:15)

SOMO LA SITA — SEHEMU YA 1

FUNDISHO:

Maombi – Kwenda kwa kina!

Tumetumia kiasi cha muda wa ziada tukizungumzia somo la maombi. Wakati mwigine tunasita kuomba kwasababu tunajihisi kuwa hutustahili. Wakati mwingine hatufahamu la kusema na tunajiuliza jinsi ya kulisema kwasababu tumelelewa katika hali ya kufahamu kuwa kuna mfumo fulani wa kuomba. Mashindano mengine yanayofanya maombi yasiwezekane ni kwamba tumesikia wengine wakiomba, inawezekana ni

kanisa, au luninga, au mfumo fulani wa jamii na tunajiruhusu kuwa na mawazo ya hofu kwamba wengine watahukumu mazungumzo yetu na Mungu.

Yatupasa kuiweka maanani kuwa maombi yanaimarisha na kuboresha mahusiano yako na Mungu. Muda wetu katika maombi hutufanya tuwe watu wa kutegemewa na kuaminiwa mbele za Mungu. Maombi hutufanya tuwe karibu na Mungu na kuingia kwenye uwepo wake.

Mtume Paulo kwenye nyaraka zake, anashirikisha kanisa baadhi ya maombi yake, ambao ni mfano wetu sisi kuwa tunaweza kujiombea na kuombea watu wengine pia. Kwanza, furahia kusoma maombi haya ambayo yameandikwa kwa kanisa mojawoja ambayo Paulo aliyafahamu. Soma maombi hayo tena na kumbuka jinsi ambavyo ungeomba maombi haya kwa maisha yako mwenyewe. Mwisho usome maombi kama mambi unayoombea wengine.

ZOEZI:

Rejea ya Biblia, Maombi ya Paulo kwa ajiri ya maombi yako, maombi yako kwaajili ya wengine.

Mfano:

Wafilipi 1:9-11

Kwa kanisa lililoko Filipi,

Kwamba upendo wangu

uongezeke zaidi na zaidi

katika maarifa

na kina na hekima.

Kwamba uwenza wa wanangu

marafiki, (tumia jina)upendo uongezeke

zaidi katika ufahamu

Wakolosai 1:9

1 Wathesalonike 1:2-3

2 Timotheo 1:3-4

Mfano:

Waefeso 6:19

Mtume Paulo anawataka Waefeso

kumwombea

Omba kwamba ili

Nikifungua kinywa changu,

Kwa ujasiri

Nitazungumza kwa niaba ya Yesu

Kwamba wachungaji wangu,

ndugu wote wawili

watazungumza kwa ujasiri

kwa niaba ya Yesu

Kuifanya Biblia iwe yako

Kadiri tunavyoendelea kujifunza, anza kuchunguza jinsi mistari tofauti inaweza kutumiwa kuimarisha maisha yako ya maombi. Daftari yako itakuwa mahali pa kuangalia kwa ajiri yako kutunza kumbukumbu ya vifungu, na kukuruhusu kurejea nyuma kwenye kifungu wakati wako wa maombi.

SOMO LA SITA— SEHEMU YA 2

FUNDISHO: Maombi

Kuhitimisha hii sehemu muhimu ya utangulizi kuhusu maombi, hebu tuangalie baadhi ya maombi yaliyoandikwa kwenye Biblia. Tumia kalamu yako kuweka alama kwenye maneno na sentensi kwenye kifungu chenyewe ambacho ni cha maana kwako. Usijali kuwa hufahamu kila kitu ambacho mtu ameweka kwenye maombi yake. Hilo si lengo la zoezi hili. Hii ni fursa tu ya kugundua maombi ya wengine ambayo yamewekwa kwenye Biblia, na kujifunza tofauti mbalimbali ambazo maombi yanaweza kusemwa.

ZOEZI:

Rejea ya Biblia. Ni nani anayeomba?

Neno lenye maana, sentensi au mstari kwaajiri yako.

2 Samweli 22:2-51

1 Wafalme 8:22-53

Mwanzo 18:22-33

Yohana 2:3

Mathayo 26:39

Luka 23:42

SOMO LA SITA — SEHEMU 3

FUNDISHO:

Kugundua mazoea inaweza kuwa kichekesho. Baadhi ya vifungu na simulizi zilinazo patikana kwenye Biblia ni za kuchekesha.

. Kwa mfano , luninga na mikanda ya sinema imetufanya tufahamu kuhusu Kutoka na utoaji wa Amri Kumi.

ZOEZI:

Mazoezi kwa masomo lilobakia kwa juma hili limeandaliwa kukupatia fulsa ya kuonyesha na kujisomea mwenyewe hizi makala ulizozoea, mistari na simulizi. Unahitaji kuzingatia mahali ambapo kifungu kimeandikwa, weka alama kwenye Biblia yako kwa rejea ya baadae, na jiandikie kitu kipya au kilichokuvutia ambacho umegundua au swali ambalo umeibua.

Japokuwa maswali yako yameachwa pasipo majibu kwa sasa, unaweza kuyatunza kwaajiri ya baadae. Tumia kalamu ya rangi kuyawekea alama kwenye kolamu ya kwanza ambayo umegundua. Furahia usomaji wako! Jaribu kukumbuka ambako ulijifunza au ulikosikia hadithi au tukio. Sawa, Hebu tuanze!

Waraka/simulizi/tukio Tukio la kumbukumbu ya ki-Biblia mapendekezo ya mtu bibafsi. Amri Kumi

Kutoka 20:1-17;

Kumbukumbu 5:1-22

a.

b.

Sala ya Bwana

Mathayo 6:5-15

Luka 11:1-4

a.

b.

Zaburi ya tatu

Zaburi 23

a.

b.

Hotuba ya mlimani

Mathayo 5:3-12

a.

b

Sura ya Upendo

1 Wakorintho 13:4-13 a.

b.

SOMO LA SITA — SEHEMU YA 4

ZOEZI:

Simulizi na matukio yalizoelieka zaidi.

Nyaraka/Simulizi/matukio

Rejea za Biblia

Mawazo na mapendekezo ya mtu binafsi

Yohana 3:16, 17

Yohana 3:16, 17

a.

b.

Muujiza wa kwanza wa Yesu
Yohana 2:1-11

a.

b.

Danieli katika shimo la simba
Danieli 6:1-28

a.

b.

SOMO LA SITA ~ SEHEMU YA 5

ZOEZI:

Bado simulizi na matukio yaliyozoeleka

Nyaraka/simulizi/matukio

Rejea za Biblia

Mawazo na mapendekezo ya mtu binafsi

Kuzaliwa kwa Yesu

Luka 2:1-20

a.

b.

Agizo kuu

Mathayo 28:16-20

a.

b.

ZOEZI:

Ikiwezekana orodhesha baadhi ya simulizi nyingine, matukio, au rejea za nyongeza za Biblia ambazo zimezoeleka kwako. Tumia zana za itifaki na jaribu kuonyesha mahali ambapo vumbuzi hizi nyingine zinapatikana kwenye Biblia.

MARUDIO

Hili SILO zoezi! Wakati mwingine inatia moyo kutathimini kujifunza kwa mtu. Tunajiamini zaidi na tunashawishika kuendelea mbele. Umemaliza kujifunza Biblia kwa kichwa cha somo ***Kuifanya Biblia Kuwa Yako***.

Hebu tukumbuke mambo ambayo umekuwa ukifanyia kazi kwa majuma haya yaliyopita:

- Watambue Waandishi wa Biblia, makukusudi, na asili
- Jua Lugha ya asili
- Nafasi ya kitabu katika Agano la Kale na Agano Jipya
- Fahamu mpangilio wa vitabu vya Biblia katika makundi yake
- Tofautisha mifumo mbalimbali ya uandishi
- Kuonyesha nyaraka ulizozoea, paseji, na simulizi
- Kuthamini matumizi ya zana katika kujifunza Biblia.
- Kutumia zana kupitia Biblia nzima kwa mazingira husika
- Kuendeleza ukuaji wa orodha ya msamiati.
- Kuongeza uchaguzi wa mistari iliyokaririwa
- Kukuza ufahamu juu ya maombi
- Kutenga muda kila siku kwa ajiri ya kujifunza
- Kuthamini mahusiano na mwanafunzi mwingine
- Kukua kila siku na mwanafunzi mwingine

Matokeo mengine ya msingi yameonekana kwa sababu umejifunza mbinu au nidhamu:

1. Umeongeza ufahamu wa Biblia kama kitabu.

2. Umefundishwa kutumia ipasavyo baadhi ya zana.
 3. Umefanya maamuzi juu ya ratiba yako .
 4. Umeunganishwa na wanafunzi wengine wenye moyo wa kujifunza.
- Hongera!Umekuwa mtu mwenye kujitoa, umejizatiti, Umeunganishwa na kukamilika
Msafiri katika Kitabu!

Table of Contents

Type chapter title (level 1)	1
Type chapter title (level 2)	2
Type chapter title (level 3)	3
Type chapter title (level 1)	4
Type chapter title (level 2)	5
Type chapter title (level 3)	6